MID WEEK JACKPOT!
TZS. 544,830,140
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**JK ataka Watanzania kumwombea Rais Samia**

UKURASA 3


BUFE
IJUMAA APRILI 14, 2023 Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
UTT, yafanikiwa 'kuchanja' uwekezaji mtaji kwenye kundi la taifa la kesho
UCHUMI
Kilio cha vijana kukosa ajira, mada inayomuibukia Mwigulu mkutanoni
• Kila mwaka, vyuo vinamwaga milioni moja

UKURASA 11

# Nipashe

Ijumaa Aprili 14, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581280

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

rdian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



# Spika aipa mzigo serikali ushoga

• **Ataka** ichunguze ukubwa wa tatizo, Majaliwa atoa neno... *Endelea ukurasa 2*



Mamalishe wakifanya biashara katika mazingira hatarishi kutokana na majitaka yaliyotuama na kutoa harufu mbaya katika soko la Mabibo, jirani na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa afya zao na wateja wao. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### SERIKALI YASIMAMISHA MIKOPO HALMASHAURI

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa ameagiza mamlaka za serikali za mitaa nchini kusitisha utoaji wa fedha za mikopo kwa vijana, wanawake na watu wenye...

UKURASA WA 4

### WASOMEWA MASHTAKA 460 KWA SAA TANO

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, imetumia saa tano kwa kuwasomea mashtaka 460 wafanyakazi wawili wa Kampuni ya Usafirishaji ya Usangu...

UKURASA WA 5

### SERIKALI YATOA UFAFANUZI KIKOKOTOO ASILIMIA 33

SERIKALI imetoa ufafanuzi kuhusu matumizi ya kanuni ya asilimia 33 ya kikokotoo cha mafao kwa wastaafu, ikisema lengo la kutumika kwake ni...

## 'Wanafunzi wanaougua Himofilia wasichapwe'

UKURASA 3



# LHRC yataja mikoa sita vinara mauaji ya wanandoa

UKURASA 2

**MICHEZO** NABI AMKABIDHI MAJUKUMU BACCA UK.24

**KATUNI** UK.6




Wananchi wakiangalia gari iliyofeli breki na kuingia kweye mtaro, katika barabara ya Mbezi-Goba, mkoani Dar es Salaam jana. Hakuna aliyejeruhiwa katika ajali hiyo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Spika aipa mzigo serikali ushoga

**Na Godfrey Mushi,**
DODOMA

BUNGE limeagiza serikali kufanya utafiti wa kina kuhusu ukubwa wa tatizo la ushoga na mambo gani ambayo taifa linataka kwa sasa yaongezeke kwenye Sheria ya Makosa ya Kujamiiana (SOSPA) ya mwaka 1998 na Sheria ya Kanuni ya Adhabu ili Bunge litakapotaka kutunga sheria liwe linaelewa tatizo ni kubwa kiasi gani kwenye jamii.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alitoa agizo hilo wakati akijibu mwongozo ulioombwa jana na Mbunge wa Arumeru Magharibi (CCM), Noah Lemburis, aliyetaka Bunge kusema neno kuhusu mjadala wa kupinga vitendo vya ushoga na mapenzi ya jinsia moja unaoendelea sasa maeneo mbalimbali.

Katika maelekezo yake, Spika Dk. Tulia aliagiza Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Maendeleo ya Jamii na Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania (LRCT), kufanya utafiti ni mambo gani yanayotakiwa yaongezwe kwenye sheria kuondoa upungufu unaolalamikiwa.

"Jambo alilolizungumzia Mheshimiwa Lemburis ni kweli limekuwa kwenye mjadala mrefu sana hapa Bungeni na imefikia pahala wako wabunge, nafikiri kwa hisia zile zikazidi sana, wakawa wanatumia lugha ambayo haipendezi sana kusemwa hapa Bungeni.

"Kwa muktadha huo, mijadala ambayo imeendelea hapa ndani nafikiri ni kwa sababu moja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya bajeti huwa inahusu mambo mengi; kimsingi mambo yote yaliyoko kwenye jamii. Kwa namna mjadala wetu ulivyojadiliwa, nafikiri sote tunakubaliana kwamba jambo hili limeshasikika na limeshaeleweka.

"Tumesikia wananchi wakilizungumzia na viongozi wetu wakilizungumzia, viongozi wa dini, viongozi wa kiserikali pia wamelizungumzia. Kwa muktadha huo, serikali imeelewa kitu gani kinapaswa kufanyika kwenye jambo hili.

Lakini sote tunafahamu yako mambo ambayo sisi kwa ufahamu wetu tunayafahamu kwamba yanatokea sehemu nyingine lakini hapa kwetu yapo ambayo ni mabaya sana, yanatokea huko kwingine lakini hapa kwetu hayajafika," alisema.

Dk. Tulia pia alisema anafikiri kadri vitendo hivyo vinavyozungumzwa na wao Wabunge wasije kujikuta wanayakaribisha kwa kufungua wigo wa kuyazungumza kwa namna nyingine, moja kwa matumizi ya lugha, kwa sababu chombo hicho ni cha wananchi, wanatazana watu wazima na watoto; hivyo ni lazima pale wanapotaka kufanya jambo litakuwa la faida zaidi kwa wananchi ambao wanawawakilisha kuliko kuleta uharibifu zaidi.

Alisema katika nchi, sheria hutungwa kulingana na mazingira, akitolea mfano Sheria ya Makosa ya Kujamiiana na Sheria ya Makosa ya Jinai, zina vifungu vinavyohusu jambo hilo.

"Sasa ikiwa yako mapungufu kwenye hivyo vifungu ambavyo viko kwenye sheria, tunayo Tume ya Kurekebisha Sheria, ambayo inaweza kulifanyia jambo hilo kazi; na ili tutoke tukiwa tumeelewana vizuri, waheshimiwa wabunge tujue michango yetu imeshachukuliwa na upande wa serikali,

"Mimi sasa kwa niaba yenu waheshimiwa (Wabunge), niagize serikali, Wizara ya Katiba na Sheria, ikishirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini pia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, ambayo pia inashughulika na mambo haya na mambo ya ndani ya nchi, muone namna ya kufanya utafiti, kupitia hii Tume ya Kurekebisha Sheria, muone ni mambo gani ambayo tunataka yaongezeke kwenye sheria ili yale mapungufu yasiwapo.

"Tunataka kutunga sheria, tukiwa tunaelewa tatizo ni kubwa kiasi gani kwenye jamii yetu, maana watu hapa tunasema tu, limeongezeka kiasi gani hatujui. Ni kubwa sana, ni kubwa sana, kwa kiasi gani hatujui," alisisitiza na kusema jambo hilo wameshawakabidhi serikali walifanyie kazi na Bunge kama chombo cha kutunga sheria, litatunga sheria hiyo kulingana na taarifa hiyo ambayo serikali itakuwa wameipata.

**NDUMBARO AANIKA TATIZO**

Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, alisema sheria dhidi ya maadili zipo na ni kali na kuwa changamoto iliyopo ni utekelezaji wake.

"Sheria hizi zipo tangu mwaka 1934 na tulifanya marekebisho mwaka 1959 na tukafanya mabadiliko makubwa zaidi mwaka 1998 kupitia Sheria ya Makosa ya Kujamiiana, hivyo sheria zipo na kali, ikibidi tuifanyie marekebisho zaidi,"alisema.

**MAJALIWA AJIBU**

Wakati akihitimisha mjadala wa makadirio ya ofisi yake, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema serikali imepokea hoja na michango mbalimbali ya wabunge na itaelekeza Tume ya Marekebisho ya Sheria, kuzipitia sheria hizo, kuzifanyia utafiti kwa kina na kitaalamu ili kufanya marekebisho.

"Wakati tunaendelea na mjadala wa hoja hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu, wabunge wengi walionyesha kukerwa na uwapo wa matukio mbalimbali yanayokinzana na utamaduni, mila na desturi zetu. Matukio na matendo haya yamekuwa yakihatarisha uimara na ustawi wa familia zetu na mustakabali wa taifa kwa ujumla.

"Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa, nchi yetu inazo sheria kali tu na sheria zetu zote zinasimamia kila eneo na pia zinakataza bayana hivyo na zimewekwa adhabu mbalimbali kwa makosa ya namna hiyo na yale ya udhalilishaji kwa watoto ikiwemo ulawiti." alisema

Waziri Mkuu, alisema ziko pia sheria zinazokataza kuweka kwenye mitandao maudhui yanayochochea uhusiano wa aina hiyo na mmomonyoko wa maadili yetu ikiwamo Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura 16, ambayo inatamka bayana vitendo vya mapenzi ya jinsia moja au kinyume na maumbile, iwe kwa faragha au kinyume na makubaliano ni kosa la jinai.

Alisema sheria hiyo pia inakataza udhalilishaji wa watoto kwenye matendo yanayofanana na hayo pamoja na kuweka adhabu kwa kosa la kujaribu kufanya vitendo vilivyokatazwa chini ya sheria husika.

"Mbili, kanuni za maudhui mtandaoni, chini ya Tangazo la Serikali namba 558 la mwaka 2020, linakataza kuweka mtandaoni maudhui yenye kuonyesha mahusiano (uhusiano) ya (wa) jinsia moja, sambamba na adhabu zake.

"Tatu, iko sheria ya makosa ya kimtandao sura namba 22 inazuia kutangaza au kusababisha machapisho ya ngono au kutumia matusi kwa kompyuta au mfumo wowote wa kiteknolojia," alisema.

# LHRC yataja mikoa sita vinara mauaji wanandoa

**Na Elizabeth Zaya**

RIPOTI ya Haki za Binadamu ya mwaka 2022 iliyotolewa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), imetaja mikoa sita iliyoongoza kwa matukio ya mauaji ya wenza.

Matokeo ya utafiti huo uliofanywa katika mikoa 20 ya Tanzania Bara, imeitaja mikoa hiyo na idadi ya matukio kwenye mabano kuwa ni Mtwara (sita), Dar es Salaam (manne), Shinyanga, Dodoma na Katavi matatu kila mmoja.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, sababu kubwa iliyochangia vitendo hivyo vya mauaji ya wenza kwa mkoa wa Dar es Salaam ni kutokana na idadi kubwa ya watu.

Pia katika mikoa mingine iliyotajwa katika ripoti hiyo, sababu za mauaji zinatokana na kuendelea kushikilia mila na desturi zilizopitwa na wakati.

Akizungumza na Nipashe jana mkoani Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Dk. Anna Henga, alisema kutokana na matukio hayo, kuna haja ya kuchukua hatua za haraka za kupambana na tatizo hilo.

"Na tunapongeza kuanzishwa kwa madawati haya ya jinsia yanaoendeshwa na Jeshi la Polisi, matukio mengi yanaripotiwa huko. Kwa mfano Kanda ya Ziwa wao ndio walikuwa wa mwanzo kuanzisha madawati hayo na tumeona yamesaidia sana katika utoaji wa taarifa," alisema.

Henga alisema miongoni mwa mapendekezo yaliyotolewa na kituo hicho baada ya utafiti wa ripoti hiyo ni kutaka kufanya zaidi uchunguzi kwa sababu zinazochangia matukio hayo kufanyika.

"Mara nyingi tunashuhudia watu wanauawa lakini inachukuliwa kawaida tu, hili si jambo la kuchukuliwa kawaida, kuna haja ya kuanza kuchukua hatua zaidi," alisema.

Pia alisema kituo chao kinapendekeza kutungwa kwa sheria ya kupinga vitendo hivyo vya ukatili wa kijinsia.

"Lakini pia, kuwekwe utaratibu wa kuundiwa kanda maalum maeneo ambayo yanakithiri kwa matukio ya namna hiyo, kama ambavyo tumewahi kushuhudia baadhi ya maeneo wamefanya hivyo pale yalipoonekana yamekithiri," alisema.

Henga alisema wanaamini kwamba kwa kufanya hivyo kutasaidia kupambana na matukio hayo.

Katika ripoti hiyo ilionyesha kuwa, vyombo vinavyoaminiwa zaidi katika utoaji wa haki na utatuzi wa migogoro ni viongozi wa dini asilimia 70, vikao vya familia asilimia 60, Asasi Zisizo za Kiserikali (AZAKI) na watoa msaada wa kisheria asilimia 59, mwenyekiti wa kijiji asilimia 41, viongozi wa kimila asilimia 39, mahakama asilimia 38, mabaraza ya kata asilimia 29 na polisi asilimia 19.

# ‘Wanafunzi wanaougua Himofilia wasichapwe’

**Na Christina Mwakangale**

CHAMA cha Himofilia Tanzania, kimesema changamoto wanazopata wazazi na walezi wa watoto wanaougua ugonjwa huo, wanaosoma shule za umma ni adhabu ya viboko shuleni jambo linalowasababishia kuvimba, kupata vidonda na damu kuvuja na kuhatarisha uhai wao.

Himofilia ni ugonjwa unaosababisha chembechembe ndogo za kuzuia damu kuganda au kuzikosa na mtu asipotibiwa huweza kupata ulemavu, kiharusi au kifo.

Mwenyekiti wa wanawake wanachama wa chama hicho, Regina Valence, ambaye pia watoto wake wawili wanaugua ugonjwa huo, alisema wazazi wanakumbana na changamoto kadhaa ikiwamo adhabu za shuleni kwa watoto pamoja na mabinti zao kuingia siku za hedhi nyingi, isivyo kawaida.

“Watoto wetu wanaosoma shule za kawaida tu hizi za umma, wanachapwa, wanavimba na damu kuivilia ndani. Wengine wanatokwa vidonda na wakivuja damu kwa hili tatizo haigandi. Tunaomba serikali iwaangalie watoto wa himofilia wasichapwe shuleni,” alisema Regina.

Alisema chama hicho chenye wanachama 200 kutoka maeneo tofauti nchini, wanapokutana na kuzijadili changamoto, wamebaini zinalingana hasa uchumi duni, kunyanyapaliwa na watoto wao kukua kwa muda mrefu.

“Tunatengwa na jamii, familia zinatutelekeza, waume pia. Wagonjwa wa himofilia wanahitaji uangalizi, watoto wanavimba magoti, viwiko na wa kike wakiingia siku zao za hedhi huwa ni nyingi na kusababisha kulazwa na kukosa masomo darasani,” alisema Regina.

Mtoto anayeugua ugonjwa huo, Edson Praygod (10), alisema aligundulika akiwa na umri wa mwaka mmoja, na alichelewa kufanyiwa tohara hali iliyosababisha kuchekwa na wenzake.

“Nilishtuka kwanza, nikamuuliza baba, mama maswali mengi. Na hata nilipofanyiwa tohara mwaka jana, niliogopa ila nilitiwa moyo. Ila mwanzo nilijisikia aibu kwa sababu wenzangu walifanyiwa tohara mapema walinicheka,” alisema Edson.

Mkurugenzi wa Utafiti na Mafunzo, Dk. Jessie Mbwambo kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), alisema ugonjwa huo ulianza kugundulika mwaka 2018 na tiba yake ni ghali.

“Tangu uhuru himofilia ilianza kugundulika kwa maana ya utambuzi na tiba mwaka 2018. Tunashukuru mradi kuwafikia wagonjwa, kuwagundua na kuwatibu. Ugonjwa huu ni miongoni mwa magonjwa ya damu ikiwamo selimundu,” alisema Dk. Mbwambo.

Mratibu wa Mradi wa Himofilia nchini, Dk. Stella Rwezaura, alisema mradi huo ulianza Novemba 2020 kwa kutekelezwa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), sasa umezifikia hospitali za kanda na rufani huku matarajio ni kuzifikia kila mkoa.

“Mradi unalenga kuwa na kanzidata, kuwaibua wagonjwa na kuwatibu. Kliniki sita zimefunguliwa ikiwamo KCMC, Bugando, Hospitali ya Kanda ya Rufani Mbeya, Benjamin Mkapa, mkoani Dodoma hivi karibuni tutakwenda Kigoma na Zanzibar,” alisema Dk. Rwezaura.

Meneja Mkuu wa Shirika la Novo Nordisk Haemophilia, Denise Braendgaard, alisema mradi huo unatekelezwa kwenye nchi mbili Tanzania na Kenya yenye kliniki tisa huku nchini zikiwa sita.

Daktari wa magonjwa ya damu kutoka MNH, Gurishael Walter, alisema ugonjwa wa himofilia huwaathiri zaidi wanaume na kwa mujibu wa takwimu za kitaalamu kwenye kila watu 100,000 mmoja anaugua (sawa Watanzania 6,000 kati ya milioni 60) na 200 pekee ndiyo waliogundulika na kuanza tiba.

# JK ataka Watanzania kumwombea Samia

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

RAIS mstaafu Dk. Jakaya Kikwete, amesema Watanzania wanatakiwa kuendelea kuiombea nchi iendelee kuwa tulivu na pia Rais Samia Suluhu Hassan aweze kutafutia majibu ya vikwazo vinavyowakabili wananchi.

Alitoa kauli hiyo wakati akizungumza na waumini wa dini ya kiislamu, viongozi wa serikali, watoto yatima, wajane na wadau wa maendeleo wa Mkoa wa Pwani katika iftari iliyoandaliwa na Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakari Kunenge.

Kunenge, aliandaa futari hiyo Ikulu ndogo mjini Kibaha kwa niaba ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Kikwete, alimshukuru Rais Samia kwa kuwakumbuka watoto yatima na wajane kwa kuwapa futari hiyo kwakuwa jamii hiyo inapaswa kutunzwa na watu wote.

Alisema, kitendo cha kuandaa futari hiyo ni kumtukuza Mungu hasa kuwasaidia yatima ambao mahitaji yao yanategemea misaada ya wahisani mbalimbali.

Alimpongeza Mkuu wa Mkoa wa Pwani kwa kazi nzuri anayofanya ndani ya mkoa kwa kuwa amekuwa kiongozi anayejali maendeleo ya mkoa kiuchumi.

Kunenge alisema, ameandaa futari hiyo kwa niaba ya Rais Samia na lengo kubwa ni kuwakutanisha yatima na wajane

Alisema yatima 150 na wajane 50 wameshiriki futari hiyo na kuwaasa wazazi kuwatunza watoto wao katika maadili yanayofaa ili wasijiingize katika vitendo vilivyo kinyume na utamaduni wa Tanzania.

Aliwataka watumie fursa zilizopo kufanya shughuli za kilimo ili wajiongezee kipato na kwa watumishi wa serikali kuacha ufisadi na kufanyakazi kwa uadilifu.

Shekhe Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Hamis Mtupa, aliwaonya wanaoandika miradi kwa ajili ya kuomba fedha kwa za watoto yatima kuacha kutumia kichaka hicho kwa ajili ya maslahi yao.

Alisema wapo baadhi ya watu wanaotumia watoto yatima kama mtaji wa maisha yao na wanapopata fedha hizo hutelekeza watoto hao na hatimaye kuangalia maslahi yao jambo ambalo halimpendezi Mungu.


Bank of India (Tanzania) Ltd.

Relationship beyond banking

**Fully owned subsidiary of Bank of India (Public Sector Bank)**

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA

**IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DESEMBA 2022
Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Mwaka wa sasa 31-DES-22 | Mwaka Uliopita 31-DES-21 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 2,431 | 1,905 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 16,418 | 16,405 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 48,465 | 51,033 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 1,144 | 1,663 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 8,378 | 23,972 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 98,855 | 70,515 |
| 12 | Mali Nyingine | 2,310 | 2,548 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Kodi iliyoahirishwa | 104 | 74 |
| 16 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 2,570 | 3,021 |
| **17** | **JUMLA YA MALI** | **180,675** | **171,136** |
| B. | **B. DHIMA** | | |
| 18 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 60,327 | 57,932 |
| 19 | Amana za Wateja | 76,795 | 70,619 |
| 20 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 21 | Amana Maalumu | - | - |
| 22 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 31 | 28 |
| 23 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 25 | 25 |
| 24 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 3,281 | 2,588 |
| 25 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 26 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 27 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 28 | Dhima Nyingine | 1,823 | 2,436 |
| **30** | **JUMLA YA DHIMA** | **142,282** | **133,628** |
| **31** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **38,393** | **37,508** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,500 | 21,500 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 2,499 | 1,631 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 13,509 | 12,860 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 885 | 1,517 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **38,393** | **37,508** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 15,807 | 21,443 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 4,871 | 2,080 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 773 | 638 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 21.25% | 21.92% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 4.89% | 2.92% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 72.66% | 55.35% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali | 54.71% | 41.20% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 86.18% | 85.03% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 6.67% | 5.80% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 5.57% | 5.74% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOSHIA 31 DESEMBA 2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Mwaka wa sasa 31 Des 2022 | Mwaka Uliopita 31 Des 2021 |
|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 13,396 | 12,691 |
| 2 | Gharama za Riba | (5,369) | (4,713) |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **8,027** | **7,979** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 54 | 198 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (1,565) | (1,165) |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **998** | **869** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 180 | 166 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 818 | 702 |
| | 6.3 Gawio | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | - | - |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(5,766)** | **(5,431)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (2,665) | (2,233) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | (257) | (256) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (2,843) | (2,942) |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **1,747** | **2,449** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (862) | (932) |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **885** | **1,517** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa robo ya mwaka /mwaka** | **885** | **1,517** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 34 | 32 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 41 | 71 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 2 | 2 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.02% | 1.49% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 2.33% | 4.11% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 40.06% | 40.05% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 5.44% | 5.68% |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2022

| | Mtaji wa Hisa | Malipo Juu ya bei ya Hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2022** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2022** | 21,500 | - | 14,378 | 1,630 | - | - | **37,508** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 885 | - | - | - | 885 |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (869) | 869 | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31.12.2022** | **21,500** | - | **14,394** | **2,499** | - | - | **38,393** |
| **Mwaka uliopita 2021** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2021** | **21,500** | - | **12,012** | **2,479** | - | - | **35,991** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 1,517 | - | - | - | 1,517 |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 848 | (848) | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31.12.2021** | **21,500** | - | **14,378** | **1,630** | - | - | **37,508** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Mwaka wa sasa 31 Des 2022 | Mwaka uliopita 31 Des 2021 |
|---|---|---|---|
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 1,747 | 2,449 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | |
| | - Hasara Katika Mali nyinginezo | - | - |
| | - Hasara na Kuchakaa Katika Mali | 205 | 530 |
| | - Mikopo iliyofutwa na Tengo la mikopo | 19 | 2 |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 8,571 | 7,043 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (28,567) | (467) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (4,186) | 66 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 632 | (489) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 556 | (488) |
| | -Mabadiliko Halisi mikopo ya muda mrefu itolewayo na mabenki mengine | 1,143 | 5,056 |
| | - Kodi Iliyolipwa | (925) | (876) |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | ***(20,804)*** | ***12,826*** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (362) | (271) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | ***(362)*** | ***(271)*** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | - | - |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | |
| | **Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | **(21,165)** | **12,555** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka / Mwaka | 45,094 | 32,539 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka / Mwaka** | **23,928** | **45,094** |

**BANK OF INDIA (TANZANIA) LTD**
**DAR ES SALAAM**

**Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Mr. Antaryami Sarangi<br>Mkurugenzi Mtendaji | Imesainiwa | 31.03.2023 |
| Mr. Mahadhil M. Karwani<br>Mkuu wa Fedha | Imesainiwa | 31.03.2023 |
| Mr. Allen Richard<br>Mkaguzi Mkuu wa Ndani | Imesainiwa | 31.03.2023 |

**Hapo juu ni baadhi ya taarifa kutoka katika ukaguzi wa taarifa ya fedha ya benki kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba 2022, na zimeandaliwa kwa kulingana na sera za kimataifa (IFRS). Taarifa hizi za fedha zimekaguliwa na mkaguzi aliyeidhinishwa RSM Eastern Africa na zimepata hati safi.**

**Taarifa hii ya fedha imepitishwa na Bodi ya Wakurugenzi na imesainiwa na wakurugenzi wafuatao kwa niaba ya wenzao**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| 1. Dr. Benard E. Mnzava- Mkurugenzi | Imesainiwa | 31.03.2023 |
| 2. Mr. Suitbert Kageuka - Mkurugenzi | Imesainiwa | 31.03.2023 |

HABARI KITAIFA




Mkurugenzi wa Biashara na Masoko wa Vodacom Tanzania, Linda Riwa akizungumza na mawakala wa mauzo wa kampuni hiyo, wakati wa uzinduzi wa programu maalum ya tuzo kwa mawakala hao ikiwemo kujishindia safari ya kwenda Afrika ya Kusini, kupitia kampeni mpya inayojulikana kama 'Zaidi ya Mtandao', jijini Dar es Salaam na mikoa mingine nchini kote jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yasimamisha mikopo halmashauri

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa ameagiza mamlaka za serikali za mitaa nchini kusitisha utoaji wa fedha za mikopo kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kwa miezi mitatu, kutokana na kuandaliwa kwa mfumo mpya wa utoaji mikopo hiyo.

Akijibu hoja za wabunge walizotoa kwenye mjadala wa hotuba ya makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2023/24, Majaliwa alisema hatua hiyo imetokana pia na maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu matumizi mabaya ya fedha hizo.

Majaliwa alisema kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wabunge kuhusu kiasi kidogo cha fedha za mikopo kinachotolewa kwa makundi maalum hayo kutokidhi matakwa ya kuyainua makundi hayo kwa kufanya shughuli za uzalishaji au biashara.

Aidha, alisema baadhi ya halmashauri hutoa fedha hizo kwa watumishi wa halmashauri au wakati mwingine vikundi hewa badala ya walengwa na kusababisha fedha za mikopo hiyo kutorejeshwa.

"Nazielekeza halmashauri kote nchini kusitisha utoaji wa fedha za mikopo hiyo zinazotokana na makusanyo ya ndani kuanzia Aprili hadi Juni, 2023 wakati serikali inajipanga kuwa na mfumo mpya wa utoaji wa mikopo hiyo," alisema.

Akizungumzia hoja ya wakurugenzi wa halmashauri kwamba wanatumia fedha za Mfuko wa Jimbo kinyume cha sheria, Majaliwa aliagiza wakurugenzi hao kuheshimu na kuzingatia vipaumbele vinavyopitishwa na Kamati ya Mfuko wa Jimbo na kuhakikisha matumizi ya fedha hizo yanazingatia Sheria ya Mfuko wa Jimbo na Sheria ya Ununuzi wa Umma.

"Nimwelekeze Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kuhakikisha maofisa ununuzi kwenye halmashauri hawawi kikwazo katika kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele vya matumizi ya fedha za Mfuko wa Jimbo hususan upatikanaji wa vifaa kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi ya Umma.

"Mbunge ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Mfuko wa Jimbo inayoratibu miradi na shughuli zitakazotekelezwa kupitia mfuko huo, na pia ndiye mwenye mamlaka ya kuitisha vikao vya kamati hiyo. Kwa upande wake, Kamati inalo jukumu la kupokea, kujadili na kupitisha vipaumbele vya matumizi ya fedha za Mfuko wa Jimbo kama ilivyokubaliwa," alisema.

Kuhusu hoja ya taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Waziri Mkuu aliliambia bunge kuwa serikali haitamfumbia macho yeyote atakayebainika katika matumizi mabaya ya fedha na mali za umma na kuwa hatua kali zitaendelea kuchukuliwa.

Alisema taarifa ya CAG imeainisha baadhi ya maeneo ambayo yalikuwa na viashiria vya usimamizi usioridhisha wa mali na fedha za umma na maeneo hayo ni pamoja na matumizi mabaya ya mikopo ya halmashauri, kasoro za utekelezaji wa miradi na baadhi ya mifumo kutosomana.

"Nitumie fursa hii kuliarifu bunge lako tukufu kwamba baada ya ripoti hiyo kuwasilishwa Bungeni, tayari Serikali kwa upande wake imeanza kuifanyia kazi mara moja," alisema.

Majaliwa alisema baadhi ya hatua zinazoendelea kuchukuliwa na serikali kuwa ni kuhakikisha maofisa masuhuli wote wanaandaa majibu ya hoja, kama inavyoelekezwa katika Sheria na Kanuni za Ukaguzi wa Umma na kusisitizwa na Rais Samia.

# Wasomewa mashtaka 460 kwa saa tano

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, imetumia saa tano kwa kuwasomea mashtaka 460 wafanyakazi wawili wa Kampuni ya Usafirishaji ya Usangu Logistics, likiwamo la wizi wa Sh 428,030,000.

Wafanyakazi hao ni Katibu Muhtasi Tamal Rashid (24) na Meneja wa Kituo cha Kampuni hiyo, Salim Salim (37), wote wakazi wa Dar es Salaam.

Mashitaka hayo yalisomwa jana na jopo la mawakili watano wa serikali likiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi Grace Mwanga mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Amri Msumi, kuanzia saa 6:00 adhuhuri hadi 11:00 jioni.

Mwanga alidai kuwa washtakiwa hao wanatuhumiwa kula njama, kughushi na kuwasilisha nyaraka za uongo 229 kwa mtu aliyefahamika kwa jina na Brigita Banda kwa lengo la kujipatia kiasi hicho cha fedha.

Alidai kuwa washtakiwa hao walighushi nyaraka 229 za malipo na kuonyesha kwamba ni halisi na zimetiwa saini na wakurugenzi wa kampuni hiyo, Hydar Ismail na Sadkhan Ismail, huku wakijua si kweli.

Inadaiwa kuwa washtakiwa baada ya kughushi nyaraka hizo, waliziwasilisha kwa Banda kwa ajili ya malipo ya Sh. 428,030,000 huku wakijua nyaraka hizo ni za kughushi.

Mwanga alidai kuwa washtakiwa hao ambao walikuwa waajiriwa katika kampuni hiyo, walitenda makosa hayo kati ya Desemba 23, 2021 na Novemba 6, 2022 katika eneo la Tabata Matumbi ndani ya wilaya ya Ilala, Dar es Salaam.

Katika shitaka la 460, washitakiwa wanadai kuwa katika tarehe hizo zilizotajwa, wakiwa waajiriwa wa Usangu Logistics, waliiba Sh. 428,030,000 wakiwa eneo la Tabata Matumbi, Dar es Salaam.

Baada ya kusomewa mashitaka hayo, washtakiwa walikana kuhusika na madai hayo, hivyo mahakama kuwataka kuwa na wadhamini wawili na kila mmoja aweke Sh. 214,015,000.

Hakimu Msumi alisema kama mdhamini atashindwa kuweka fedha hiyo, basi atatakiwa kuwasilisha hati ya mali isiyohamishika yenye thamani hiyo na pia hawatatakiwa kutoka nje ya mkoa wa Dar es Salaam bila kibali cha mahakama.

Washitakiwa hao walitimiza masharti hayo ya dhamana kwa kuwasilisha mahakamani hapo hati na ripoti ambayo inaonyesha thamani ya majengo.

Hata hivyo, Wakili wa Serikali Neema Moshi aliomba mahakama iteue mtu wa kwenda kwenye wizara husika ili kujiridhisha uhalali wa hati hizo licha ya kwamba zina ripoti ya thamani.

Hakimu Msumi aliahirisha kesi hiyo hadi leo kwa ajili ya hatua hiyo ya kujiridhisha hati hizo na washtakiwa walirudishwa mahabusu.


**INVITATION FOR BIDS (IFB)**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**MINISTRY OF NATURAL RESOURCES AND TOURISM (MNRT)**

**Project: Selous Ecosystem Conservation and Development Programme (SECAD)**

**(KfW Contract Reference No.:2012 66 451)**

14th April 2023

1. The **Government of the United Republic of Tanzania** through the Ministry of **Natural Resources and Tourism (MNRT)** has received a grant from the German **State-owned Investment and Development Bank (KfW) towards the costs of implementing the Selous Ecosystem Conservation and Development Programme (SECAD),** and intends to apply part of the proceeds towards payments under the contract for the **Construction of one (1) Classroom and one (1) Female Dormitory for Likuyu Sekamaganga (Community Based Conservation Training Center (CBCTC) and Rehabilitation of Chingoli Wildlife Management Area (WMA) Head Office Building.**

2. The **Ministry of Natural Resources and Tourism (MNRT)** now invites sealed bids from eligible and qualified bidders for the construction works comprised of the following package.

| Package Number | Tender Number | Lot Number | Lot Description |
|---|---|---|---|
| 001 | MNRT/GOPA/CBCTC &WMAPP13 | PP13 | Construction of Classroom and Female Dormitory for Likuyu Sekamaganga CBCTC and Rehabilitation of Ching'oli Wildlife Management Area (WMA) Headquarter Building |

3. Bidding will be conducted by means of the National Competitive Bidding (NCB) procedure with the qualification as specified in the KfW Guidelines for Procurement of Goods, Works and associated Services in Financial Cooperation with Partner Countries ("KfW Guidelines"

**https://www.kfw-entwicklungsbank.de/PDF/Download-Center/PDF-Dokumente-Richtlinien/FZ-Vergaberichtlinien-V-2021-EN.pdf).**

4. A complete set of the bidding documents **(in English)** is available to interested eligible Bidders upon the submission of a written application to the address below and upon payment of a non-refundable fee of ***Tanzanian Shillings One Hundred Thousand only (TZS 100,000.00).*** The method of payment is via bank deposit to the following account at **Tanzania CRDB bank - Account name: Selous Ecosystem Conservation and Development with Account number 0150555174201**

   The documents shall be sent by Courier (related costs to be covered by the interested Bidder) or physical pickup by the Bidders at ***Ministry of Natural Resources and Tourism (MNRT), c/o GOPA, Mpingo House, 4th Floor, Room No. L406, PO Box 25295, 40 Julius Nyerere Road, Dar es Salaam, Tanzania.***

5. Bids in one original plus two paper copies and one digital copy, properly filled in, and enclosed in plain envelopes must be delivered to the address below: ***SECAD Project Manager, Ministry of Natural Resources and Tourism (MNRT), c/o GOPA, Mpingo House, 4th Floor, Room No. L406, PO Box 25295, 40 Julius Nyerere Road, Dar es Salaam, Tanzania*** on or before ***Thursday 19th May 2023*** at ***12:00hours EAT***. Electronic bidding will not be permitted and late bids will be rejected. Bids will be publicly opened in the presence of the bidders' or designated representatives and anyone who choose to attend at the address below on ***Thursday 19th May 2023 at 14:00 hours*** at ***MNRT Room No. L406.***

**Ministry of Natural Resources and Tourism (MNRT)**
**c/o GOPA, Mpingo House, 4th Floor, Room No.L406, PO Box 25295,**
**40 Julius Nyerere Road, Dar es Salaam, Tanzania.**
**Contact:- Adreherm Nziku (MNRT) / Comfort Mosha (GOPA)**
**Email:- adreherm.nziku@tawa.go.tz / Comfort.Mosha@gopa-infra.de**

## HABARI KITAIFA

# Serikali yatoa ufafanuzi kikokotoo 33%

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

SERIKALI imefafanua kuhusu matumizi ya kanuni ya asilimia 33 inayopigiwa kelele kwenye sakata la kikokotoo cha mafao ya wastaafu, ikisema lengo la kutumika kwake ni kutaka kuwakutanisha katikati wale waliokuwa wanapata asilimia 50 na wale wa asilimia 25.

Aidha, imesema kanuni hiyo imeongeza mafao ya mkupuo kwa wanachama milioni 1,364, 050, sawa na asilimia 81 ya wanachama wote waliokuwa wanapata asilimia 25.

Jana, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, wakati anajibu hoja za Wabunge waliochangia mjadala wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, alisema ulipaji wa mafao ya wastaafu nchini umeimarika kwa kiwango kikubwa.

Kwa mujibu wa Waziri Ndalichako, changamoto zilizokuwa zinasababisha wastaafu wasilipwe kwa wakati, serikali ya awamu ya sita imezifanyia kazi.

"Changamoto kubwa iliyokuwapo ilikuwa ni ukwasi; kulikuwa na deni la wafanyakazi walioirithiwa kutoka kwenye Mfuko wa PSPF (Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma), ambao wafanyakazi kabla ya mwaka 1999 walikuwa hawachangii. Kwa hiyo, serikali ilipowaingiza kwenye mfuko iliahidi kuwalipia michango kiasi cha shilingi trilioni 4.6 na serikali ya awamu ya sita, tayari imetoa shilingi trilioni 2.17," alisema.

Amelihakikishia Bunge kuwa mifuko ya hifadhi ya jamii, imeimarisha mifumo yake ya ulipaji mafao kwa wastaafu na wanalipa kwa wakati ndani ya muda uliowekwa kisheria.

Kuhusu kikokotoo, Prof. Ndalichako ameweka wazi kuwa kanuni ya kukokotoa mafao kwa watumishi wa umma, ambayo ilianza kutumika Julai mosi, 2022, imetokana na sheria namba mbili ya mwaka 2018 ya mifuko ya hifadhi ya jamii, ambayo imeanzisha Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), iliyounganisha mifuko minne ya GEPF (Mfuko wa Taifa wa Mafao ya Watumishi wa Serikali), LAPF (Mfuko wa Pensheni), PPF (Mfuko wa Pensheni kwa Mashirika ya Umma) na PSPF (Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Serikali).

Waziri Ndalichako alisema, "Kabla ya kuunganisha mifuko ilikuwa na kanuni tofauti za ulipaji wa mafao, Mfuko wa GEPF, PPF ulikuwa unalipa mafao ya mkupuo ya asilimia 25 na Mfuko wa LAPF na PSPF, ulikuwa unalipa mafao ya mkupuo ya asilimia 50, lakini Mfuko wa NSSF (Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii), ulikuwa unatoa mafao ya mkupuo ya asilimia 25."

Katika majibu yake, Waziri huyo, alisema baada ya mifuko kuunganishwa kulikuwa na uwianishaji kanuni, na mwaka 2018 ziliundwa kanuni za kutekeleza sheria hiyo ambazo ziliweka watumishi wote walipwe mafao ya mkupuo ya asilimia 25.

"Kanuni ilivyoanza kutumika wale waliokuwa wanalipwa asilimia 50 hadi 25 waliona wameshushwa pa kubwa na kukawa na malalamiko, na serikali ilisitisha na kukaa na wafanyakazi na ikaja na kanuni ya asilimia 33, Kanuni hii lengo lake ilitaka kuwakutanisha katikati wale waliokuwa wanapata asilimia 50 na wale wa asilimia 25," alisisitiza

# Bweni shule wavulana Green Valley lateketea kwa moto

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

BWENI la wavulana wa shule yenye mchepuo wa Kiingereza ya Green Valley, jijini Arusha, limeteketea kwa moto usiku wa kuamkia juzi na kusababisha uharibifu mkubwa wa mali za wanafunzi na shule.

Akizungumzia tukio hilo, Mkurugenzi wa shule hiyo, Yahaya Njarita, alisema hakuna mwanafunzi aliyedhurika na janga hilo zaidi ya vifaa vyao vya shule kuteketea na baadhi kuokolewa.

Alisema bweni hilo lilianza kuteketea majira ya saa nne asubuhi na chanzo hakijajulikana.

Kwa mujibu wa mashuhuda wa tukio hilo, waliona moshi ukitoka katika moja ya vyumba vya bweni hilo na kupiga kelele zilizosaidia wanafunzi kujikusanya kwa kushirikiana na wafanyakazi na kuanza jitihada za kuzima moto huo.

"Unajua shule yetu huwa tunatoa mafunzo ya kuzima moto, baada ya kuwapo kwa taarifa hiyo moja kwa moja wanafunzi kwa kushirikiana na majirani tulianza kuzima na baadaye Jeshi la Zimamoto na uokozi walifika na kufanikisha kuzima moto huo," alisema Njarita.

Alisema bweni hilo lenye vyumba vitatu, hulaza wanafunzi 75, lakini walioripoti baada ya shule kufunguliwa jana ni 15 ambao hata hivyo wakati moto ulipozuka walikuwa darasani.

Mrakibu wa Jeshi la Zimamoto na uokozi na Kamanda wa Mkoa, Osward Mwanjejele, alisema kuwa jeshi hilo lilipokea taarifa ya wito wa tukio hilo majira ya saa 4.54 asubuhi na kufika eneo la tukio wakati moto ukiendelea kuwaka kwa kasi kubwa.

Alisema walifanikiwa kuzima moto huo huku sehemu kubwa ya jengo na mali za wanafunzi zikiteketea kwa sababu ya mazingira magumu ya kuzima moto kutokana na ufinyu wa eneo.

Alisema chanzo cha moto huenda ikawa hitilafu ya umeme kutokana na jengo hilo kuonekana kuwa la zamani na kutofanyiwa marekebisho mfumo wa waya za umeme.

"Taarifa za awali zinaonesha moto ulitoka juu ya dari na hii inaweza kuwa hitilafu ya umeme iwapo kama mfumo wa waya za umeme haujafanyiwa marekebisho kwa muda mrefu kwa kuwa sheria za Zimamoto zinataka mfumo wa waya za umeme ufanyiwe marekebisho kila baada ya miaka 15," alisema Mwanjejele.

Baadhi ya wazazi, Joseph Emmanuel na Agness Amos, walisema wanamshukuru Mungu baada ya kufika eneo la tukio na kukuta watoto wakiwa salama.


MWANGA HAKIKABANK

## MWANGA HAKIKA BANK LIMITED
## MINIMUM DICLOSURE OF CHARGES AND TARIFFS

| PRODUCTS/ SERVICES | BUSINESS CURRENT A/C | PREMIUM CURRENT A/C | PERSONAL SAVING A/C | SALARY A/C | MTOTO SAVING A/C | JIPANGE SAVING A/C | WEKEZA GROUP A/C | MALENGO SAVING A/C | FOREX ACCOUNT USD & EURO | JIWEKEE SAVING A/C | MHB PAMOJA A/C | MSOMI ACCOUNT |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Account opening | 100,000.00 | 50,000.00 | 20,000.00 | 0 | 10,000.00 | 10,000.00 | 20,000.00 | 100,000.00 | 10 | 0 | 50,000.00 | 10,000.00 |
| Minimum operating Balance | 100,000.00 | 50,000.00 | 10,000.00 | 5,000.00 | 5,000.00 | 0 | 10,000.00 | 100,000.00 | 10 | 10,000.00 | 50,000.00 | 5,000.00 |
| Interest Payable | N/A | N/A | 3.00% | 3.00% | 6.00% | 2.00% | 3.00% | 2% < 10Mil, 4%>=10Mil | 0.50% | 2.00% | 2% | 3.00% |
| Interest bearing amount | N/A | N/A | 50,000.00 | 50,000.00 | 50,000.00 | 50,000.00 | 50,000.00 | 100,000.00 | 5,000.00 | 20,000.00 | 500,000.00 | 20,000.00 |
| Monthly Mantainance fee | 20,000.00 | 10,000.00 | 2,500.00 | 2,500.00 | Free | Free | Free | Free | 2 | Free | Free | Free |
| Deposit | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free |
| Monthly Statement | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free |
| Adhock statement Per page | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 1 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 |

### OTHER CHARGES

| SERVICES | AMOUNT ( TZS) |
|---|---|
| Certificate of Balance | 30,000.00 |
| Confirmation to the Auditors | 30,000.00 |
| Search for information above 5 years | 15,000.00 |
| Cheque book cost (Per Leaf) | 600.00 |
| Status report | 30,000.00 |
| Stop payment order | 30,000.00 |
| Dishonoured cheque for lack of funds or refer to drawer or effect not cleared | 100,000.00 |
| Dishonoured cheque due to the technical error caused by customer | 60,000.00 |
| Dormant Account Activation | Free |
| Account Closing on Customer Demand | 10,000.00 |
| Counter cheque per leaf [Within the Bank] | 15,000.00 |
| Salary Processing fee [ per Transaction] | 1,000.00 |
| Customer ID | 10,000.00 |
| Pre-Mature breaking of Fixed Deposit on customer request | Minimum of 50% of the accrued interest |
| CCTV Camera footage searching request from Customer | 30,000.00 |
| Uncollected Cheque Book/Destruction | 5,000.00 |
| Visa Card Issuance-Classic | 10,000.00 |
| Visa Card Issuance-Gold | 15,000.00 |
| Replacement Visa Card-Classic | 15,000.00 |
| Replacement Visa Card-Gold | 25,000.00 |
| Umoja Card Mantainance fee | 1000 per month |
| Visa Card- Classic Mantainance fee | 3,000 per QTR |
| Visa Card-Gold Mantainance fee | 5,000 per QTR |
| Uncollected ATM Card | 5,000.00 |
| PIN reset fee | 5,000.00 |
| Withdraw fee local (Umoja ATM) | 1000-99,000=1500 100,000-400,000=1700 |
| Withdraw fee other Bank (Domestic Banks) | 3,500 |
| Withdraw fee other Bank (International) | 11,000 |
| Balance inquiry Umoja ATM | 300 |
| Balance inquiry other Domestic Banks | 950 |
| Balance inquiry other Bank (International) | 2,000 |
| Decline Domestic [Insufficient fund] | 1,000 |
| Decline International [Insufficient Balance] | 1,500 |
| QR transactions | 3% of Transaction Amt |
| POS transactions | 3% of Transaction Amt |
| E-commerce transactions | 3% of Transaction Amt |

**Cash Withdraw Over the Counter [TZS/ USD/EURO]**

| TRANSACTION AMOUNT | RATES |
|---|---|
| Wekeza/Jiwekezee | 2,000.00 |
| Bellow 10 Mil | 3,000.00 |
| Above 10Mill to 50 Mil | 0.10% |
| Above 50Mil t0 100 Mil | 0.090% |
| Above 100Mil to 300 Mil | 0.089% |
| Above 300 Mil | 0.079% |

**Cash Withdraw Over the CounterForeign Currency [USD/EURO]**

| TRANSACTION AMOUNT | RATES |
|---|---|
| Below USD/EURO 4,000 | 2 |
| Above USD/EURO 4000 | 0.1% more than USD/EURO 40 |

### AGENCY BANKING CHARGES

| TYPE OF SERVICES | RATES |
|---|---|
| Deposit | Free |
| Balance Inquiry | 500 |
| Min Statement | 700 |
| Transfer of fund within MHB | 2,000 |
| Transfer of funds to other Bank | 13,000 |

### AGENCY BANKING WITHDRAWAL FEE

| AMOUNT | FEE |
|---|---|
| Up to 50,000 | 850.00 |
| 50,000 - 100,000 | 1,000.00 |
| 100,000 - 300,000 | 2,000.00 |
| 300,000 - 500,000 | 3,500.00 |
| 500,000 - 1,000,000 | 4,500.00 |
| 1,000,000 - 3,000,000 | 6,000.00 |
| 3,000,000 - 5,000,000 | 10,000.00 |

### MOBILE BANKING CHARGES

**WITHDRAWAL CHARGES**

| MINIMUM [TZS] | MAXIMUM [TZS] | RATES [TZS] |
|---|---|---|
| 0 | 10,000 | 800 |
| 10,001 | 19,999 | 1,800 |
| 20,000 | 49,999 | 3,500 |
| 50,000 | 99,999 | 5,200 |
| 100,000 | 199,999 | 7,200 |
| 200,000 | 499,999 | 8,200 |
| 500,000 | 999,999 | 10,500 |
| 1,000,000 | 2,000,000 | 11,200 |
| 2,000,001 | 3,000,000 | 12,000 |
| 3,000,001 | 5,000,000 | 15,000 |

**FUND TRANSFER CHARGES**

| | |
|---|---|
| Transfer of Funds within MHB | 2,000.00 |
| Transfer of funds to other Banks | 13,000.00 |

### EFT/SWIFT/TISS

| | |
|---|---|
| EFT within the Bank (Incoming) | Free |
| EFT to other Banks | 1,500.00 |
| TISS Transfer | 10,000.00 |
| T.T. Transfer | - |

### STANDING ORDER

| | |
|---|---|
| Instructions within MHB | FREE |
| Standing Order to other Bank | 10,000/= |

www.mhbbank.co.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ushauri wa Makamu wa Rais kwa Mahakama utekelezwe

**MAKAMU** wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Philip Mpango ameishauri Mahakama nchini kujielekeza kufanya maboresho yenye kupunguza urasimu na kupunguza gharama za uendeshaji wa mashauri, husussani ya madai ili wananchi waweze kupata huduma za utoaji haki kwa gharama nafuu.

Pamoja na maboresho makubwa iliyofanya na inayoendelea kufanya, bado kuna maeneo mengine yanayopaswa kufanyiwa kazi ikiwamo gharama kubwa za kuendesha mashauri ya madai.

Kadhalika, kuna baadhi ya malalamiko yanayotolewa na wananchi kuhusu uwapo wa vitendo vya rushwa kwa baadhi ya maofisa wa Mahakama na ameshauri kufanyia kazi hisia za wananchi kuhusu suala hilo na kuziba mianya na viashiria vyote.

Hata hivyo, maboresho ya Mahakama katika matumizi ya TEHAMA yameleta ufanisi na imeshauriwa kutoa mafunzo kwa watumishi wa kada za chini ili kuendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia yanayoendelea duniani.

Ili iweze kufanyakazi zake kwa ufanisi zaidi Mahakama imetakiwa kuendelea kusogeza huduma zake za Mahakama za Mwanzo ili kuwafikia wananchi kwa ukaribu zaidi.

Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Hamis Juma anasema lengo la kukutana kwa watendaji wa mahakama ni kutathmini kama huduma zao zimekidhi matarajio ya wananchi wa Tanzania kutokana na maboresho yaliyofanyika.

Kikao hicho pia kitatathmini namna Mahakama ilivyotimiza matarajio ya Serikali ya Tanzania na Benki ya Dunia kuhusu maboresho ya utoaji haki ambayo ilizisukuma hadi kufikia makubaliano ya kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 91 zitumike katika maboresho kuanzia Februari 2022 hadi Desemba 2025.

Majaji, Mahakimu na Wamiliki wa Mradi wa Maboresho ya Mahakama, wameelekezwa kutoishia kujitathmini kwa kuhesabu idadi ya mashauri yaliyokamilishwa, bali kutathmini utendaji wa haki unaozingatia vigezo vilivyotajwa katika Ibara ya 107A (2) ya Katiba (1977).

"Tunapofanya tathmini ya huduma zetu ni vyema kuzingatia takwa la kikatiba, yaani kuzingatia sheria wakati wa kusikiliza na kutoa uamuzi; kutenda haki kwa wote bila kujali hali ya mtu kijamii au kiuchumi; kutochelewesha haki bila sababu ya kimsingi, kukuza na kuendeleza usuluhishi baina ya wanaohusika katika migogoro; na kutenda haki bila kufungwa au kupita kiasi na masharti ya kiufundi.

Hata hivyo, katika suala la rushwa, Jaji Mkuu amesema bado Mahakama ina changamoto kadhaa ikiwamo tuhuma za rushwa.

Matarajio ya wananchi ni kupata huduma bora zisizo na hisia au viashiria vya rushwa na ameagiza watumishi na viongozi wote wa Mahakama kufanya tathmini ya uhalisia, mianya, vipenyo, viashiria na mitazamo ya rushwa.

Pia, kuhusu utekelezaji wa mradi wa maboresho hadi kufikia Desemba 2022, mlundikano wa mashauri mahakama umepungua kutoka asilimia 11 kwa mwaka 2021 hadi kufikia asilimia sita mwezi Desemba, 2022, kiwango cha kumaliza mashauri kiliongezeka kutoka asilimia 78 mwaka 2021 hadi kufikia 84 mwezi Desemba, 2022.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# Pongezi sana serikali kwa mradi huu wa maji Makongo- Bagamoyo

**MWEZI** uliopita Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa aliandika historia kwa wakazi wa Dar es Salaam Kaskazini, kwa kuzindua mradi mkubwa wa kusambaza maji kutoka Makongo, hadi Mji wa Bagamoyo unaotarajiwa kuhudumia wananchi takribani 450,000.

Ni mradi uliokuwa ukisubiriwa kwa hamu kubwa na wakazi wa maeneo ya wilaya ya Kinondoni, ikiwamo Changanyikeni, Goba, Mivumoni, Mbweni, Madale, Tegeta A, Bunju, Wazo, Ocean bay na Salasala, Mabwepande, Mbopo, Kinzudi na Kilongawima, umeleta nuru mpya kwa wakazi hao na kurejesha imani kwa Serikali mara baada ya kuanza kupata huduma ya maji.

Wakazi wa Mataya, Sanzale, Migude, Ukuni, Mtambani, Nianjema, Kimara Ngo'mbe, Kisutu, Block P, Mapinga, Vikawe, Vikawe bondeni na maeneo jirani, ni sehemu ya wanufaika wakuu wa mradi huo.

Uzinduzi wa mradi huo umeleta unafuu mkubwa kwa wakazi wa maeneo tajwa ambao awali hawakuwa na huduma ya maji kwa muda mrefu hususani wakazi wa Bunju, Madale, Mivumoni, Mbopo, Salasala na Goba.

Haya ni maeneo ambayo yamekuwa kwenye changamoto ya ukosefu wa maji kwa muda mrefu, kutokana na kutokuwepo mtandao wa maji wa kusambaza huduma kwa wananchi wanaoishi katika maeneo hayo.

Kukosekana huduma ya maji kwa wananchi hawa, kulisababisha baadhi ya wakazi kutumia gharama kubwa ya kutafuta maji mbali na makazi yao.

Ukamilishwaji mradi huu uliotekelezwa chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), ni mojawapo ya mafanikio makubwa yaliyofikiwa na serikali ya sasa, chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kuweza kuwatua ndoo kichwani wananchi wanaonufaika na mradi huu.

Utekelezaji wa kasi wa mradi huo, umechagizwa kwa asilimia kubwa na jitihada za Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuwezesha kupatikana shilingi bilioni 65.4 kutoka kwa Benki ya Dunia, ambao ni washirika wa maendeleo fedha ambazo zilitumika kutekeleza mradi huu na kukamilika kwa asilimia 100.

Mradi ulihusisha ujenzi wa matenki matatu ya kuhifadhi maji yaliyojengwa kwenye maeneo ya Vikawe, Mbweni na Tegeta A yenye ujazo wa lita milioni tano kila moja. Pia, kuna ujenzi wa vituo viwili vya kusukuma maji vilivyopo Vikawe na Mbweni, ujenzi wa mtandao wa mabomba madogo na makubwa ya kusafirisha na kusambaza maji ya kuanzia inchi 2.5 hadi inchi 16 kwa umbali wa 1,252.

Akizindua mradi hivi karibuni, Waziri Mkuu alinukuliwa akisema, serikali inatambua changamoto ya maji iliyokwepo kwenye maeneo haya na ndiyo maana Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alifanya uamuzi wa dhati kusukuma utekelezaji wa mradi huu ili wananchi mpate maji.

Pamoja na kuipongeza DAWASA kwa kazi kubwa iliyofanyika, pia aliiagiza DAWASA kwa kuwaambia kuwa mradi umekamilika na kazi iliyopo sasa ni kuhakikisha wananchi wote wanafanyiwa maunganisho ya maji kikamilifu ili kila mmoja aone manufaa ya mradi huu nyumbani kwake kwa kupata maji.

Mbali na hapo, Majaliwa aliwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa serikali kwa kulinda na kutunza vyanzo vya maji pamoja na mazingira, kwa kuwa kuharibu mazingira ni hujuma.

Mbali na wananchi miradi hii ya maji huwa na manufaa kwa wananchi, pia imekuwa na manufaa makubwa kwa wawekezaji kwani wakipata maji ya uhakika shughuli za uzalishaji mali viwandani zinapata msukumo hivyo kusaidia ukuaji wa uchumi.

Ni kwa muda mrefu maji yamekuwa yakisumbua kwenye baadhi ya maeneo ya Jiji la Dar es Salaam na Mkoa wa Pwani lakini kasi inayoonyeshwa na DAWASA, kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya maji inatia moyo kwamba shida ya maji sasa kwenye maeneo hayo inakwenda kuwa historia.

Wakati serikali inafanya jitihada za kuhakikisha shida ya maji kwenye maeneo mengi inakuwa historia ni wajibu wa wananchi nao sasa kuwa walinzi wa miundombinu hiyo inayojengwa kwa gharama kubwa.

Wananchi wanapaswa kutoa taarifa kwa watu wanaojaribu kuharibu miundombinu ya maji ili wachukuliwe hatua za kisheria ili hatimaye miradi hiyo iweze kuwa endelevu kwa vizazi na vizazi na kamwe wasikubali kuona inahujumiwa.

# DAWASA kuboresha upatikanaji maji Dar

**Na Joseph Mwendapole**

KAMPUNI ya ujenzi ya Metito ya Misri, imesaini mkataba wa kusanifu, kujenga na kuendesha mtambo mpya wa kuchakata majitaka katika eneo la Mbezi Beach, mkoani Dar es Salaam, katika mradi unaotekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali na Benki ya Dunia (WB).

Mradi huo unaotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), unatarajiwa kuchangia kuboresha usafi wa mazingira kwa kuwezesha majitaka kukusanywa na kutibiwa kikamilifu.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Kiula Kingu, alisema mwishoni mwa wiki kuwa mtambo huo wa kisasa utakaojengwa eneo la Mbezi Beach wilayani Kinondoni, utakuwa na uwezo wa kuchakata lita milioni 16 za majitaka kwa siku.

"Upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira unaweza kuchangia kuleta maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii katika Mkoa wa Dar es Salaam. Tumeiamini Metito ikiwa ni moja kati ya kampuni bora ulimwenguni ili kutekeleza mradi huu wa ujenzi wa mtambo wa kuchakata majitaka Mbezi Beach na kuongeza kuwa Mamlaka inaamini mtambo huo utaleta matokeo chanya kwa uchumi na jamiii utakapoanza kufanya kazi," alisema Kingu.

Alisema Mtambo utatumia teknolojia ya kisasa ili kupunguza gharama za uendeshaji na matengenezo na kuongeza ubora wa uchakataji wa majitaka.

Aidha, alisema mtambo huo unatarajiwa kutumia eneo dogo, lakini utawezesha kuchakata majitaka kwa ubora zaidi na kwa gharama nafuu.

"Pamoja na usanifu na ujenzi wa mtambo, wigo wa mkataba kati ya kampuni ya Metito na DAWASA unahusisha miaka mitatu ya uendeshaji na usimamizi wa mtambo huo wa kuchakata majitaka kwa kushikiriana kwa karibu na wataalamu na watumishi wa DAWASA katika maeneo yote ya uendeshaji," alisema.

Alisema mtambo huo utakuwa na teknolojia ya kisasa pamoja na mifumo ya kibiolojia ya kuchakata takatope, ili kuzalisha gesi asilia itakayotumika katika uendeshaji wa mtambo na hivyo kupunguza matumizi ya umeme kwa asilimia 40 katika mtambo.

Alisema mifumo ya kibiolojia itatumika katika awamu ya kwanza ya uchakataji ili kuhakikisha ubora wa takatope na kwamba Tanzania imeazimia na kuweka malengo ya kuongeza upatikanaji wa huduma za majisafi kwa kupitia mpango wa maendeleo endelevu - lengo namba sita (majisafi na usafi wa mazingira ifikapo 2030) uliowekwa na Umoja wa Mataifa.

Alisema mtambo wa kuchakata majitaka utachangia maendeleo endelevu katika Mkoa wa Dar es Salaam, hususani katika sekta ya uchumi na viwanda kwa kuwezesha upatikanaji wa nafasi za ajira kwa wataalamu pamoja na kulinda afya na ustawi wa jamii kwa patikanaji wa huduma stahiki ya usafi wa mazingira.

Akizungumzia ushindi wa zabuni hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Metito Africa, Karim Madwar, alisema mradi huo ni hatua muhimu ya kuboresha mifumo ya usafi wa mazingira katika Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na kuimarisha udhibiti wa miundombinu huku ikizingatia ulinzi wa mifumo ya ikolojia. "Kanuni za Metito ni Athari, Uendelevu na Uvumbuzi ambazo zimezingatiwa katika mradi huu tuna furaha kufanya kazi na DAWASA katika utekelezaji wa mradi huu na tunatarajia mradi huu uwe wa mfano wa miradi mingine kama hii katika eneo hili la Afrika," alisema.

Mkataba wa mradi wa Mbezi Beach ulisainiwa hivi karibuni huku ujenzi ukitegemewa kuanza mwezi Aprili, 2023 na kukamilika Oktoba 2024.



Kaimu Shekhe wa Mkoa wa Dar es Salaam, Walid Al-hadi Omar (kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa BancABC Tanzania, Imani John wakiwaongoza wateja na wageni waalikwa katika futari iliyoandaliwa na benki hiyo kwa wateja wake, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Walilia serikali barabara ya Malinyi-Ifakara itengenezwe

**Na Idda Mushi,** MALINYI

WATUMIAJI wa barabara ya Malinyi-Ifakara wakiwamo wasafirishaji wa bidhaa wameiomba serikali kutafuta suluhisho la kudumu kuitengeneza barabara hiyo kutokana na kukwama mara kwa mara barabarani kwa sababu ya mvua inayoendelea kunyesha nyakati za masika.

Walidai kukwama barabarani kwa kati ya siku tatu hadi nne na kuiomba serikali kuharakisha matengenezo ya kudumu ya barabara hiyo kuu inayounganisha wilaya hiyo na Halmashauri za Wilaya za Kilombero, Ulanga na Mlimba na maeneo mengine.

"Wakati mwingine kwa siku moja unatumia zaidi ya saa tisa hadi kumi kufika Ifakara kutokea Malinyi kutokana na kukwama, na magari mengine hukwama na kulala njiani, serikali ichukue hatua za haraka hata kumleta mkandarasi wa dharura kwenye maeneo korofi yanaosababisha magari kukwama, "alisema Said Sabu, mmoja wa wasafirishaji wa abiria katika barabara hiyo.

Mkazi mwingine wa Mtimbira, Mariam Nuru, alisema wanaamini kukwama kwa magari kunachangiwa na barabara hiyo kukosa mifereji, huku mito mingi ikifurika na kupeleka maji barabarani na kuziba makalavati.

Mbunge wa Jimbo la Malinyi, Antipas Mgungusi, akizungumza katika eneo la tukio, alisema maeneo makubwa korofi kutokana na kuathiriwa na mvua yapo kwenye kata za Itete, Mtimbira na mpakani mwa wilaya za Ulanga na Malinyi hali inayosababisha kukwama kwa wasafiri zaidi ya 300 wanaotumia barabara hiyo kila siku.

Hata hivyo, Mgungusi alisema amezungumza na menejimenti ya Wakala wa Barabara (TANROADS), Mkoa wa Morogoro waliomhakikishia kuwa tayari mkandarasi wa kutengeneza barabara hiyo ameshapatikana na alitarajiwa kuianza kazi hiyo Aprili 12, mwaka huu.

"Nimezungumza na watu wa TANROADS na wamesema mkandarasi tayari amekwisha patikana kwa ajili ya kufanya marekebisho hasa maeneo korofi ikiwamo eneo la msituni la Nambiga na Luhili ambapo magari yamenasa karibu siku ya nne leo," alisema.

Aliwataka wakandarasi waliopewa kazi hiyo kuripoti katika ofisi za halmashauri na madiwani kwenye kata zenye changamoto za barabara ili washirikiane kuonesha maeneo korofi kwa ajili ya ukarabati.

Meneja wa TANROADS Mkoa wa Morogoro, mhandisi Alinanuswe Kyamba, alikiri kupeleka mkandarasi kwa ajili ya ukarabati wa barabara hiyo kwa dharura hasa kipindi hiki cha mvua ya masika.


"Tayari mkandarasi ameshakwenda eneo la tukio na tayari kazi ya kufungua mifereji imekwishaanza pamoja na kukwangua tope linalosababisha utelezi na kufanya magari kukwama njiani," alisema Mhandisi Kyamba.

Aliwaasa watumiaji wa barabara hiyo kuwa na subira ya kupita hasa kipindi maji yakiwa yamejaa na kutoa taarifa za haraka kwa mamlaka husika ili washughulikie changamoto zinazojitokeza.

Hata hivyo, alisema serikali iko kwenye mpango wa kuitengeneza barabara hiyo ya Malinyi - Ifakara kwa kiwango cha lami na tayari imeshatangazwa na mipango ya tenda bado inaendelea ili kumpata mkandarasi wa kuifanya kazi hiyo.

Barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 140 imekuwa na changamoto za mara kwa mara za kushindwa kupitika kirahisi wakati wa mvua na mwaka huu baadhi ya maeneo husan kwenye kata tano zikiwamo za Itete, Mtimbira na Malinyi yameharibika kutokana na mvua inayoendelea kunyesha maeneo hayo na serikali kuamua kuijenga kwa kiwango cha lami kutakuwa suluhisho la kudumu kwa wananchi.

## KABWELA — Na Fadhili Mohammed



TANGAZO

VisionFund TANZANIA MICROFINANCE BANK LTD

# VISIONFUND TANZANIA MICROFINANCE BANK LTD

## AUDITED FINANCIAL STATEMENTS

### Report of the condition of bank pursuant to section 32(3) of Banking and Financial Institutions Act, 2006

### STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 31 DECEMBER 2022
(All amounts in millions of Tanzanian shillings)

| | | Current Year 31.12.2022 | Current Year 31.12.2021 |
|---|---|---|---|
| | | TZS | TZS |
| **A.** | **ASSETS** | | |
| 1 | Cash | 2,848.50 | 10,648.95 |
| 2 | Balances with Bank of Tanzania | - | - |
| 3 | Investment in Government securities | - | - |
| 4 | Balances with other banks and Financial Institutions | 2,678.40 | - |
| 5 | Cheques and other items for clearing | - | - |
| 6 | Inter branch float items | - | - |
| 7 | Bills Negotiated | - | - |
| 8 | Customers Liabilities for acceptances | - | - |
| 9 | Interbank Loans receivables | - | - |
| 10 | Investment in other securities | - | - |
| 11 | Loans, advances and overdrafts | - | - |
| | (Net of allowances for probable lossses) | 27,228.91 | 18,882.35 |
| 12 | Other Assets | 1,439.94 | 721.03 |
| 13 | Equity Investments | - | - |
| 14 | Underwritting assets | - | - |
| 15 | Property,plant and equipment | 2,336.12 | 2,536.82 |
| **16** | **TOTAL ASSET** | **36,531.88** | **32,789.16** |
| **B.** | **LIABILITIES** | | |
| 17 | Deposits from other banks and Financial Institutions | - | - |
| 18 | Customer deposits | 2,215.43 | 1,486.15 |
| 19 | Cash letters of credit | - | - |
| 20 | Special Deposits | 3,172.40 | 3,922.98 |
| 21 | Payments orders/transfers payables | - | - |
| 22 | Bankers' cheques and and draft issued | - | - |
| 23 | Accrued taxes and expenses payable | - | - |
| 24 | Long-term Borrowings | 4,617.50 | - |
| 25 | Inter branch floating items | - | - |
| 26 | Unearned income and other differed charges | 1,846.56 | 1,951.50 |
| 27 | Tax Payable | 107.12 | 49.90 |
| 28 | Other liabilities | 5,135.34 | 2,948.15 |
| **29** | **TOTAL LIABILITIES** | **17,094.34** | **10,358.68** |
| **30** | **NET ASSETS / (LIABILITIES)(16 minus 29)** | **19,437.54** | **22,430.48** |
| **C.** | **SHAREHOLDERS' FUNDS** | | |
| 31 | Paid up share capital | 21,200.00 | 21,200.00 |
| 32 | Capital reserves | 390.66 | 11.60 |
| 33 | Retained earnings | (2,400.69) | 971.31 |
| 34 | Others Reserve(Revaluation) | 247.57 | 247.57 |
| 35 | General provision reserve | - | - |
| 36 | Minority Interest | - | - |
| **37** | **TOTAL SHAREHOLDERS' FUNDS** | **19,437.54** | **22,430.48** |
| | | - | |
| 38 | Contingent liabilities | | |
| 39 | Non performing loans & advances | **313.09** | **499.14** |
| 40 | Allowances for probable losses | **868.43** | **936.28** |
| 41 | Other non performing assets | - | - |
| **D.** | **SELECTED FINANCIAL CONDITION INDICATORS** | | |
| (i) | Shareholders' funds to total assets | **58%** | **65%** |
| (ii) | Non performing loans to total gross loans | 1.4% | **2.5%** |
| (iii) | Gross loans and advances to total deposits | **407%** | **364%** |
| (iv) | Loans and advances to total assets | **75%** | **58%** |
| (v) | Earning Assets to total assets | **82%** | **58%** |
| (vi) | Deposit growth | **-0.4%** | **18.0%** |
| (vii) | Asset Growth | **11.4%** | **6.7%** |

### STATEMENT OF COMPREHENSIVE INCOME FOR THE YEAR ENDED 31 DECEMBER 2022
(All amounts in millions of Tanzanian shillings)

| | | Current Year 31.12.2022 | Current Year 31.12.2021 |
|---|---|---|---|
| | | TZS | TZS |
| 1 | Interest income | 12,543.52 | 11,112.79 |
| 2 | Interest expense | (172.12) | (129.95) |
| **3** | **Net interest income (1 minus 2)** | **12,371.41** | **10,982.84** |
| 4 | Bad debts written off | - | - |
| 5 | Imparement Losses on loans and advances | 592.66 | 780.92 |
| **6** | **Non interest income** | **1,271.55** | **1,056.90** |
| | Foreign currency dealings and translation gain/(loss) | - | - |
| | Fees and commisions | - | - |
| | Dividend income | - | - |
| | Other operating income | 1,271.55 | 1,056.90 |
| **7** | **Non interest expenses** | **16,365.08** | **11,200.05** |
| | Salaries and Benefits | 7,102.52 | 5,378.80 |
| | Other operating expenses | 9,262.55 | 5,821.25 |
| **8** | **Operating income /(loss)** | **(3,314.79)** | **58.77** |
| 9 | Income tax provisions | (57.22) | (202.53) |
| **10** | **Net income / (loss) after income tax** | **(3,372.00)** | **(143.76)** |
| **11** | **Other comprehensive income** | | |
| | Items that will not be reclassified to profit or loss: | | |
| | Gain on revaluation of property and equipment | - | - |
| | Related tax | - | - |
| **12** | **Other comprehensive income, net of tax** | - | - |
| | | - | - |
| **13** | **Total comprehensive income/(loss) for the year, net of taxes** | **(3,372.00)** | **(143.76)** |
| **14** | Number of employees | 401 | 275 |
| **15** | Basic Earning per share | (159,057) | (6,781) |
| **16** | Diluted earning per share | (159,057) | (6,781) |
| **17** | Number of branches | 1 | 1 |
| **18** | Number of Business Centre | 35 | 35 |
| | **PERFORMANCE INDICATORS** | | |
| (i) | Return on average total assets | -2.4% | -0.1% |
| (ii) | Return on ordinary shareholders funds | -16.5% | -0.7% |
| (iii) | Non interest expense to gross income | 130% | 101% |
| (iv) | Net Interest income to average earning assets | **54%** | **64%** |

### STATEMENT OF CASH FLOWS AS AT 31 DECEMBER 2022
(All amounts in millions of Tanzanian shillings)

| | | Current Year 31.12.2022 | Current Year 31.12.2021 |
|---|---|---|---|
| | | TZS | TZS |
| **I:** | **CASH FLOW FROM OPERATING ACTIVITIES** | | |
| | Net income / (Loss) | **(3,314.79)** | **58.77** |
| | **Adjustment for Non cash items:** | | |
| | Impairment / Amortizations | 1,082.61 | 1,316.23 |
| | Net changes in Loans and advances | (8,575.22) | (4,235.73) |
| | Gain/ Loss on sale of assets | (1.14) | 1.24 |
| | Net change in Deposits | (21.30) | 825.38 |
| | Net change in Short term Negotiable Securities | - | - |
| | Net change in other liabilities | 1,993.82 | 1,583.24 |
| | Tax paid | (210.00) | (210.00) |
| | Other | (505.97) | (7.20) |
| | **NET CASH PROVIDED / (USED) BY** | - | - |
| | **OPERATING ACTIVITIES** | **(9,551.99)** | **(668.07)** |
| **II:** | **CASH FLOW FROM INVESTING ACTIVITIES** | | |
| | Divident receivable | - | - |
| | Purchase of Fixed Assets | (514.41) | (189.24) |
| | Proceed from sale of Fixed Assets/loan portifolio | 19.23 | 2.66 |
| | Purchase of Non Dealing Securities | - | - |
| | Proceed from sale of Non Dealing Securities | - | - |
| | Others | - | - |
| | **NET CASH PROVIDED / (USED) BY** | - | - |
| | **INVESTING ACTIVITIES** | **(495.17)** | **(186.59)** |
| | | - | - |
| **III:** | **CASH FLOW FROM FINANCING ACTIVITIES** | - | - |
| | Repayments of Longterm Debt | 4,617.50 | - |
| | Proceeds from Issuance of Longterm Debt | - | - |
| | Proceeds from Issuance of Share Capital | 379.06 | - |
| | Payment of cash Dividends | - | - |
| | Net change in Other Borrowings | - | - |
| | Others | (134.64) | (16.32) |
| | **NET CASH PROVIDED / (USED) BY** | - | - |
| | **INVESTING ACTIVITIES** | **4,861.93** | **(16.32)** |
| **IV:** | **CASH AND CASH EQUIVALENTS** | | |
| | Net Increase/(Decrease) in Cash & Cash Equivalent | (5,185.24) | (870.97) |
| | Cash & Cash Equivalent at the Beginning of the Year | 10,754.46 | 11,625.43 |
| | **CASH AND CASH EQUIVALENT AT THE END OF THE YEAR** | **5,569.22** | **10,754.46** |

### STATEMENT OF CHANGES IN EQUITY AS AT 31 DECEMBER 2022
(All amounts in millions of Tanzanian shillings)

| | Share capital | Advance towards share capital*** | Property and Equipment revaluation reserve | Retained earnings | Total |
|---|---|---|---|---|---|
| | TZS'000 | TZS'000 | TZS'000 | TZS'000 | TZS'000 |
| At 1 January 2021 | 21,200,000 | 11,596 | 247,572 | 1,115,070 | 22,574,238 |
| Loss for the year | - | - | - | -143,758 | -143,758 |
| At 31 December 2021 | 21,200,000 | 11,596 | 247,572 | 971,312 | 22,430,480 |
| At 1 January 2022 | 21,200,000 | 11,596 | 247,572 | 971,312 | 22,430,480 |
| Loss for the year | - | - | - | -3,372,003 | -3,372,003 |
| Advance towards share capital | - | 379,064 | - | | 379,064 |
| At 31 December 2022 | 21,200,000 | 390,660 | 247,572 | -2,400,691 | 19,437,541 |

Chilala Hakooma
Chief Executive Officer
12 April 2023

Mr.Rogathe Godson
Chief Finance Officer
13th April 2021

Mr.Modest Kissima
Head of Internal Audit
13th April 2021

We, the under-named, non-executive members of the Board of Directors, attest to the correctness of the above statements, We declare that the statements have been examined by us and to the best of our knowledge and belief have been prepared in conformance with the instructions and are true and correct

Signed

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | Athanasia Soka ( Board Chaiperson) | Chairman | 12 Apr 2023 |
| 2 | Ms. Loyce Isanzu | Director | 12 Apr 2023 |

### ADA NA GHARAMA ZA HUDUMA

| Huduma za Kibenki | | | Gharama-Pamoja na VAT (TZS) |
|---|---|---|---|
| 1 | Kuangalia Salio-Dirishani & ATM | | 554 |
| 2 | Kuhamisha fedha | Ndani ya VFT hadi TZS1,000,000 | 944 |
| | | Ndani ya VFT zaidi ya TZS1,000,000 | 1,180 |
| | | Kwenda Benki nyingine hadi TZS10,000,000 | 3,554 |
| | | Kwenda Benki Nyingine zaidi ya TZS10,000,000 | 11,800 |
| 3 | Kutoa disrishani hadi TZS 5,000,000 | | 1,770 |
| 4 | Kutoa ATM | | 1,500 |
| 5 | Kadi ya ATM (Mpya au Kubadili) | | 5,000 |
| 6 | Gharama za mwezi (Monthly Acc maintanance fees) | Akiba Akaunti | 885 |
| | | Business Akaunti | 1,770 |
| 7 | Kufunga Akaunti | Akaunti ya Akiba, Watoto & Dunduliza | 2,360 |
| | | Akaunti ya Vikundi na Biashara | 5,900 |
| 8 | Taarifa ya Akaunti | Taarifa Fupi ATM | 720 |
| | | Miezi 0-3 | 1,180 |
| | | Miezi 3-12 | 3,540 |
| | | Miezi 12-24 | 11,800 |
| | | Miezi 24-48 | 29,500 |
| | | Miaka 3-6 | 41,300 |
| | | Zaidi ya miaka 6 | 55,400 |
| **Huduma Za Simu (Mobile banking)** | | | **Pamoja na VAT (TZS)** |
| 9 | Kujua Salio-Simu | | 118 |
| 10 | Kutoa-Simu | | Bure |
| 11 | Kuhamisha Fedha-Simu | | 118 |
| 12 | Taarifa Fupi-Simu | | 354 |
| 13 | Kubadili Number ya Siri | | 236 |

**Akaunti**

| s/n | Huduma | Kiwango cha chini | Riba Kwa mwaka * |
|---|---|---|---|
| 1 | Akiba Akaunti | 5,000 | 3% |
| 2 | Salary Akaunti | 5,000 | 3% |
| 3 | Kikundi Akaunti | 20,000 | 4% |
| 4 | Watoto Akaunti | 10,000 | 4% |
| 5 | Bussiness Akaunti | 100,000 | 3% |
| 6 | Joint Akaunti | 5,000 | 3% |
| 7 | Fixed Deposit Accounts | N/A | Kulingana na muda na Kiasi |
| 8 | Dunduliza Accounts | 10,000 | 4% |

** Riba kwa akaunti za aina zote itajilimbikiza kwa kila la siku kwa kiasi cha akiba cha TZS100,000 na kuendelea na kulipwa kila Mwezi.*

**Mikopo ya Vikundi**

| | Aina ya Mkopo | Riba Kwa Mwezi (Kiima punguza) | Riba Kwa mwaka (Kiima punguza) | Gharama ya mkopo |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mikopo ya Vikundi -Biashara group Loan | 5% | 60% | 3% |
| 2 | Mikopo ya Vikundi/Savings Group Loan | 5% | 60% | 2.5% |
| 3 | Mikopo ya Vikundi -Jiendeleze Group Loan | 4% | 48% | 3.5% |

**Mikopo Binafsi**

| | Aina ya Mkopo | Riba Kwa Mwezi (Kiima punguza) | Riba Kwa mwaka (Kiima punguza) | Gharama ya mkopo |
|---|---|---|---|---|
| 4 | Mkopo Binafsi- hadi TZS10M | 4% | 48% | 2.5% |
| 5 | Mkopo Binafsi inayozidi TZS10M Hadi TZS 20M | 3.50% | 42% | 2.5% |
| 6 | Mikopo Binafsi inayozidi TZS20M | 2.50% | 30% | 2.5% |
| 7 | Elimisha | 4% | 48% | 3.5% |

**Mikopo ya Kilimo**

| | Aina ya Mkopo | Riba Kwa Mwezi (Kiima punguza) | Riba Kwa mwaka (Kiima punguza) | Gharama ya mkopo |
|---|---|---|---|---|
| 9 | Mikopo Binafsi -Jikomboe Loan | 4% | 48% | 5% |
| 10 | Mikopo ya kikundi -Jitume | 5% | 60% | 5% |
| 11 | Mikopo ya Kikundi -Mkombozi Loan | 5% | 60% | 5% |
| 12 | Patnerships | Negotiable | Negotiable | Negotiable |

| Name and Title | Signature | Date |
|---|---|---|
| Chilala Hakooma ( Chief Executive Officer) | Signed | 17/Januari/2023 |
| Rogathe Godson (Chief Finance Officer) | Signed | 17/Januari/2023 |
| Modest Kissima ( Internal Audit Manager) | Signed | 17/Januari/2023 |

TANGAZO

# CITIBANK TANZANIA LIMITED

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2022

| | 2022 TZS '000 | 2021 TZS '000 |
|---|---|---|
| Mapato ya Riba | 38,407,812 | 30,977,650 |
| Gharama za Riba | (7,452,637) | (7,738,697) |
| **Mapato Halisi ya Riba** | **30,955,175** | **23,238,953** |
| Ada na Kamisheni | 6,645,105 | 5,144,355 |
| Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 13,855,461 | 9,486,490 |
| Faida nyingine | 1,801,422 | - |
| **Jumla ya Mapato** | **22,301,988** | **37,869,798** |
| Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (275,930) | (558,921) |
| **Jumla ya Mapato baada ya Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo** | **52,981,233** | **37,310,877** |
| Mishahara na Mafao | (11,590,205) | (9,501,523) |
| Uchakavu wa Mali | (2,070,498) | (1,947,302) |
| Gharama za kiutawala | (13,374,313) | (14,539,494) |
| | **(27,035,016)** | **(25,988,319)** |
| Faida /(Hasara) ya Uendeshaji | 25,946,217 | 11,322,558 |
| Tengo la Kodi ya Mapato | (7,884,168) | (3,758,502) |
| **Faida Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **18,062,049** | **7,564,056** |
| **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa** | | |
| – Mapato ambayo hayajakamilika | (904,471) | 373,260 |
| – Tengo la Kodi ya mapato ambayo hayajakamilika | 271,341 | (111,978) |
| **Mapato mengine baada ya kodi ya mapato** | **(633,130)** | **261,282** |
| **Jumla ya Faida iliyojumuishwa** | **17,428,919** | **7,825,338** |

### VIASHIRIO VYA UFANISI

| | 2022 | 2021 |
|---|---|---|
| Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Fedha za Wanahisa | 16.19% | 7.44% |
| Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Mali | 1.66% | 0.67% |
| Uwiano wa gharama na mapato | 50.76% | 68.63% |
| Uwiano wa mapato halisi ya riba kwa mali zinazozalisha | 3.38% | 2.48% |
| Uwiano wa Mapato yasiyo ya riba kwa Pato | 38.49% | 38.63% |
| Uwiano wa Mikopo kwa amana za wateja | 63.71% | 33.5% |
| Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 0.00% | 0.00% |
| Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 83.89% | 81.33% |
| Ongezeko la Mali | -5.33% | -13.69% |
| Ongezeko la Mikopo Halisi kwa wateja | 38.35% | -3.59% |
| Ongezeko la Amana za wateja | -27.22% | -21.36% |

### WARAKA MIZANIA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2022

| | 2022 TZS '000 | 2021 TZS '000 |
|---|---|---|
| **MALI** | | |
| Fedha Taslimu na Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 127,557,901 | 185,271,074 |
| Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | 145,185 |
| Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 280,235,001 | 444,505,925 |
| Chombo cha kifedha kinachotokana na Mali | 2,537,844 | 63,994 |
| Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 208,510,337 | 184,309,427 |
| Mikopo kwa Wateja | 425,805,033 | 307,774,460 |
| Mali Nyingine | 30,410,841 | 13,496,236 |
| Mali ya kodi ya kampuni | - | 542,960 |
| Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 6,673,546 | 7,610,392 |
| Haki ya matumizi ya mali | 3,908,199 | 4,550,643 |
| Malipo ya kodi yanayotarajiwa baadae | 4,048,248 | 3,361,494 |
| **JUMLA YA MALI** | **1,089,686,950** | **1,151,631,790** |
| **DHIMA** | | |
| Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 249,497,797 | 93,056,490 |
| Amana za Wateja | 668,372,731 | 918,403,379 |
| Chombo cha kifedha kinachotokana na Dhima | 48,723 | 7,499 |
| Dhima Nyingine | 56,409,943 | 34,347,647 |
| Dhima ya kodi ya kampuni | 214,377 | - |
| Dhima ya kukodisha | 3,592,558 | 4,130,816 |
| **JUMLA YA DHIMA** | **978,136,129** | **1,049,945,831** |
| **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 9,659,900 | 9,659,900 |
| Akaunti Nyingine za Mtaji | 1,387,489 | 2,020,619 |
| Tengo la ziada ya jumla | - | 604,577 |
| Mapato Yaliyobakizwa | 100,503,432 | 89,400,863 |
| **Jumla ya fedha za wanahisa** | **111,550,821** | **101,685,959** |
| **Jumla ya fedha za wanahisa na dhima** | **1,089,686,950** | **1,151,631,790** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2022

| | 2022 TZS '000 | 2021 TZS '000 |
|---|---|---|
| **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| Faida ya Uendeshaji | 25,946,217 | **11,322,558** |
| *Marekebisho kwa Ajili ya:* | | |
| Uchakavu wa Mali | 2,070,498 | 1,947,302 |
| Uchakavu wa haki ya matumizi ya mali | 642,444 | 642,444 |
| Faida/(hasara) ya mapato mengine yaliyojumuishwa -mali | (2,473,850) | (61,873) |
| Faida/(hasara) ya mapato mengine yaliyojumuishwa -dhima | 41,224 | (18,119) |
| Gharama za tengo katika mikopo | 275,930 | 558,921 |
| Mapato Halisi ya Riba | (30,955,175) | (23,238,953) |
| Faida/(hasara) katika kubadilika kwa thamani ya Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (121,179) | (98,001) |
| Faida juu ya uuzaji wa mali na vifaa | (1,062) | 1,051 |
| | **(4,574,953)** | **(8,944,670)** |
| **Mabadiliko katika shughuli za uendeshaji wa mali na madeni** | | |
| Uwekezaji wa Amana za Serikali | (20,357,398) | (28,981,479) |
| Mikopo Halisi kwa wateja | (115,926,857) | 12,700,771 |
| Mali Nyingine | (16,941,392) | 24,869,977 |
| Amana za benki nyingine | 155,711,956 | 92,089,424 |
| Amana za Wateja | (250,030,648) | (249,392,988) |
| Hifadhi ya chini ya kisheria | 5,684,693 | 25,844,272 |
| Dhima Nyingine | 24,647,274 | (32,708,939) |
| **Fedha iliyozalishwa kutokana na shughuli za uendeshaji** | **(221,787,325)** | **(164,523,632)** |
| Riba iliyopokelewa | 31,372,305 | 24,739,962 |
| Riba iliyolipwa | (6,601,872) | (7,544,323) |
| Riba ya kukodisha | (121,414) | (131,371) |
| Kodi iliyolipwa | (7,542,244) | (3,982,843) |
| | **17,106,775** | **13,081,425** |
| **Fedha Halisi zilizotumika kwa shughuli za uendeshaji** | **(204,680,550)** | **(151,442,207)** |
| **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji** | | |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (1,197,254) | (348,494) |
| Fedha zilizopokelewa kutokana na uuzwaji wa mali za kudumu | 64,666 | - |
| **Fedha Halisi Zilizotumika kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(1,132,588)** | **(348,494)** |
| **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha** | | |
| Malipo kwa ajili ya dhima ya kukodisha | (538,258) | (526,786) |
| Gawio lililolipwa | (10,169,934) | - |
| **Fedha Halisi Zilizotumika kwa Shughuli za Kifedha** | **(10,708,192)** | **(526,786)** |
| Kupungua kwa jumla ya Fedha Taslimu | **(216,521,330)** | **(152,317,487)** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa mwaka | 597,086,463 | 749,305,949 |
| Kubadilika kwa thamani ya Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 121,179 | 98,001 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Mwaka** | **380,686,312** | **597,086,463** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2022

| | Mtaji wa Hisa TZS '000 | Akaunti nyingine za mtaji TZS '000 | Mapato Yaliyobakizwa TZS '000 | Tengo la ziada ya kisheria TZS '000 | Jumla TZS '000 |
|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la mwanzo wa mwaka 1 Januari 2022** | **9,659,900** | **2,020,619** | **89,400,863** | **604,577** | **101,685,959** |
| Faida Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 18,062,049 | - | 18,062,049 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | (633,130) | - | - | (633,130) |
| **Jumla ya Faida iliyojumuishwa kwa mwaka** | - | (633,130) | 18,062,049 | - | **17,428,919** |
| Gawio litakalolipwa | - | - | (7,564,057) | - | (7,564,057) |
| Hamisho la Tengo la Ziada | - | - | 604,577 | (604,577) | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31 Desemba 2022** | **9,659,900** | **1,387,489** | **100,503,432** | - | **111,550,821** |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 1 Januari 2021** | **9,659,900** | **1,759,337** | **85,915,791** | **1,582,094** | **98,917,122** |
| Faida Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 7,564,056 | - | 7,564,056 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | 261,282 | - | - | 261,282 |
| **Jumla ya Faida iliyojumuishwa kwa mwaka** | - | 261,282 | 7,564,056 | - | 7,825,338 |
| Gawio litakalolipwa | - | - | (5,056,501) | - | (5,056,501) |
| Hamisho la Tengo la Ziada | - | - | 977,517 | (977,517) | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31 Desemba 2021** | **9,659,900** | **2,020,619** | **89,400,863** | **604,577** | **101,685,959** |

Taarifa hizi zilipitishwa na Bodi ya Wakarugenzi tarehe 30 Machi 2023 na kutiwa saini kwa niaba yake na::

Geofrey Mchangila
**Ofisa Mtendaji Mkuu**

Andulile Mwakalyelye
**Mjumbe wa Bodi**

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2014, na zinaonesha hali halisi.

Godwin Rutashobya
**Mkaguzi Mkuu wa Ndani**


Wilson Chola
**Mjumbe wa Bodi**

Andulile Mwakalyelye
**Mjumbe wa Bodi**



Ukurasa 12

Dereva Bajaji pekee aliyeanzia kubeba zege, bodaboda, leo anamiliki vyombo vitatu




Ukurasa 13

Kwa madudu haya ya CAG, hatua za wazi zionekane


# BUFE

IJUMAA APRILI 14, 2023

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




Ukurasa 14

## UTT, yafanikiwa 'kuchanja' uwekezaji mtaji kwenye kundi la taifa la kesho

UCHUMI

# Kilio cha vijana kukosa ajira, mada inayomuibukia Mwigulu mkutanoni

- Kila mwaka, vyuo vinamwaga milioni moja

**Na Halfani Chusi**

'DONDA ndugu' la ajira kwa vijana, linashika kasi zote. Mdau muhimu serikalini, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, naye anajikuta katika mustakabali wa kuwajibika nao, katika mkutano unaohusu kodi, akitaja mbinu za kukabili na kuwatuliza Watanzania katika hilo.

Mwigulu, mjini Dar es Salaam, anapenyeza ujumbe wake kuzitaka sekta binafsi kuisaidia serikali kwenye eneo hilo.

Anasema sekta binafsi ni nyenzo muhimu kumaliza tatizo hilo, akibainisha idadi ya wanafunzi wanaoingia kwenye soko la ajira na nafasi zilizopo serikalini ni tofauti.

Hapo anafafanua takwimu, wanafunzi wasiopungua milioni moja kila mwaka huingia kwenye soko la ajira, hivyo kuna haja ya sekta binafsi kuchangia kutanua wigo.

"Zamani mambo yote yalikuwa yanaweza kufanywa na serikali watu walikuwa hawaoni nafasi ya sekta binafsi miaka ya nyuma wanafunzi walikuwa wanapewa ajira wakiwa vyuoni, kwa sababu wasomi walikuwa wachache kuliko mahitaji kipindi hicho.

"Sasa hivi ukichukua wanaomaliza darasa la saba hawaendelei kidato cha kwanza, ukichukua wanaomaliza kidato cha nne na hawajaendelea kidato cha tano na ukachukua waliomaliza kidato cha sita na hawakuendelea vyuo vikuu.

Ukachukua wale wanaotoka kwenye vyuo vya kata ukaongeza na wale wanaomaliza vyuo vikuu unapata takribani wanafunzi milioni moja kila mwaka wanoingia kwenye soko la ajira" alisema na kuongeza;

"Mtu yeyote anayeanzisha shughuli ya uzalishaji anatakiwa aheshimike kwa kupewa ushirikiano wa kutosha kwa sababu anakuwa anatengeneza ridhiki za wengi hivyo watendaji wote walioko serikalini wanatakiwa wamkimbilie na kumpa msaada.

"Tunavyo tafakari hapa, tuitafakari na kodi na ushuru mbalimbali kama sehemu ya kukuzia uchumi, pamoja na kutoa ushauri na maoni yatakayo isaidia serikali kwenye kufanyia maboresho ya kodi" alishauri Nchemba.



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba. **PICHA: MTANDAO**

### WALIOKOSA AJIRA

Maumba Yahaya, ni miongoni wa wahitimu wa Shahada ya Ualimu, anayesema sekta binafsi zinapaswa kupewa kipaumbele kikubwa, ili kuwapa nafasi wahitimu wa ngazi mbalimbali waajiriwe.

"Kwa mfano mimi nimemaliza chuo, lakini sina ajira. Kama shule zingekuwa nyingi hata kama ningekosa serikalini, ningepata kwenye shule binafsi.

"Nguvu kubwa inahitajika, serikali inatakiwa kuwajali na kuwapa nguvu wawekezaji, ili wafanikiwe kuwekeza kwa kufanya hivyo tutamaliza kabisa tatizo la ajira," anashauri.

Remi Malunga, anaiomba serikali kuwaangalia waliomaliza vyuo mda mrefu wapewe kipaumbele akidai 'wamesota' sana mtaani naw engine wamekwishakata tamaa

"Inabidi serikali iangalie wale waliosota sana mtaani, kuna watu wamemaliza chuo tangia mwaka 2014 mpaka leo hawajaajiriwa hili linaumiza sana," analalama.

Muhitimu wa shahada ya biashara, Timothy Magembe, anaiunga mkono kauli ya serikali kuwezesha sekta binafsi kuweka sera nzuri zitakazosaidia kupunguza au kumaliza tatizo la ajira.

"Nafikiri ni jambo zuri sana serikali inapaswa kuweka sera nzuri zitakazo wavutia wawekezaji, ninaamini tatizo la ajira kupitia uongozi wa Rais samia, linaweza kwisha japo wote hatutaajiriwa serikalini> Wengi watakuwa kwenye mfumo wa ajira" anasema

### HATUA SERIKALINI

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye ulemavu, Patrobas Katambi, wakati akijibu swali bungeni kwa ajili ya changamoto hiyo, anasema serikali bado inaangalia namna ya kulimaliza.

Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inatekeleza Mkakati wa Taifa wa Kukuza Ujuzi wa Miaka 10 (2016/2017 - 2025/2026).

Ambapo Kupitia Mkakati huu, Serikali imefanya maboresho ya miundombinu na mitaala katika ngazi za Elimu ya Juu, Elimu ya Kati, na Mafunzo ya Ufundi Stadi," amesema Katambi.

Anasema, serikali inatoa mafunzo ya kuwezesha vijana walio nje ya mfumo rasmi wa mafunzo ili kumudu ushindani katika katika soko la ajira yakiwemo mafunzo ya uanagenzi.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo, mafunzo mengine ni uzoefu wa kazi kwa wahitimu; mafunzo ya urasimishaji ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi wa elimu na mafunzo (RPL).

BIASHARA

# Dereva Bajaji pekee mkoa aliyeanzia kubeba zege, bodaboda, leo anamiliki vyombo vitatu

**Na Neema Hussein,** Mpanda

BADO kuna wanaoamini kazi za udereva, kiasili bado ni ya mwanaume na sio wanawake. Wengine wanaenda mbali na imani, mwanamke yuko mbali na kazi za kiume, kwani baba ndio ndio kichwa cha familia.

Kutokana na imani hizo, wanawake wameendelea kupambana kuthibitisha hakuna kazi za kiume pekee, zao likijionyesha kwa mkuu wa nchi wa sasa.

Hapa mjini Mpanda, kuna mwanamama, Amina Hamisi mwenye umri miaka 42, akibeba jina maarufu "Mama Lao", ni mzazi wa watoto wawili, anayejishughulisha na biashara ya udereva wa Bajaji.

Anaiambia Nipashe kuwa ni kazi inayomfanya kuonekana mama mwenye uthubutu, kwani ni wa kwanza kufanya kazi hiyo ya bajaji mkoani Katavi, akijivunia kusomesha watoto na kuendesha maisha ya kila siku.

Mama Lao anasimulia safari yake ya udereva, akinena: "Nilianza na bodaboda moja, nimeendesha muda wa miaka mitatu, nikawa nimepata pikipiki zingine tatu zikawa nne hizo tatu nikaajiri vijana ,upande wa bodaboda.

"Maisha yangu hayakuwa magumu, nikazidi kujulikana. Kipindi hicho nilikuwa naitwa 'Dada bodaboda' na sio Mama Lao...Mama Lao limekuja baada ya kuanza kuendesha Bajaji, wakati nikiendelea na bodaboda, pia nilikuwa nafanya biashara ya mazao, natoa vijijini ili kuongezea hela ya bodaboda, mpaka kupata pesa ya kununua Bajaji.

"Mimi nimetoka familia ya umaskini tu, lazima niwe mkweli, lakini mpaka sasa wasionifahamu wanahisi nimetoka familia yenye hela, nawambia hapana nimetoka familia duni.



Amina Hamisi, akiwa katika Bajaji anayomiliki na kuiendesha. Pia, zipo nyingine mbili alizokabidhi kwa madereva wengine. **PICHA:NEEMA HUSSEIN**

> **Mimi ninachowaambia wanawake wenzangu wasikate tamaa, hakuna kazi ya mwanamke wala wanaume.**

"Nilianza kununua Bajaji moja, nikaanza kuendesha kwa muda wa miaka miwili nikanunua Bajaji nyingine, nikampa kijana, kwa hiyo kijana akitafuta na mimi pia natafuta, kipato kikaongezeka nikanunua Bajaji nyingine ya tatu."

"Maisha yangu kifupi ni mazuri, pia nazishukuru taasisi za kibenki zimenisaidia pale nilipokuwa nakwama hizi Bajaji mbili imenisaidia sana benki ya CRDB.

"Namshukuru Mungu ni mwanamke ninaejituma sana, sio kwamba nimepata kimiujiza, hapana! Ni kujituma na sasa nimeajiri vijana watatu wanaoniendeshea Bajaji zangu na mimi naendesha moja ya kwangu mwenyewe.

"Ndoto yangu haijatimia, nataka niendeshe magari makubwa. Nilikuwa naomba 'sapoti' ni mwanamke ninaejiamini, jasiri na ninakubali kufanya kazi yoyote bila ya kuchafua kazi na kusema 'hii ni ya mwanamke au mwanaume hapana.'

"Kuna kinadada wawili nimewafundisha kuendesha Bajaji hapa Mpanda waliniomba ushauri, kabla hawajaingia huku kwenye udereva Bajaji. Kuna mmoja aliniuliza 'dada kwanini unaendesha Bajaji, na mimi nikijaribu nitaweza? nikamwambia utaweza, kwa hiyo nikamfundisha.

"Akapata leseni akaanza kazi, lakini kutokana na hali ngumu, sa hizi naona wamepumzika, kwa sababu mabosi usipowaletea hela wanakunyang'anya Bajaji. Sio kwamba wameshindwa, hapana ni hali ngumu sababu wananyang'anywa hadi wavulana.

"Mimi ninachowaambia wanawake wenzangu wasikate tamaa, hakuna kazi ya mwanamke wala wanaume. Kazi kama hizi, hakuna watu wanaaminiwa kama wanawake. Mimi hizi zimeniinua sana, sa hizi nina mwaka wa nne naendesha Bajaji hapa Mpanda.

"Natamani sana niendelee katika suala hili la udereva. Ningekua na elimu, ningesema niombe hata kuendesha ndege au kuendesha treni, ila sikuweza kufika huko kutokana na familia duni niliyotokea.

"Changamoto zipo na kudharauliwa ni kawaida, isipokuwa wewe ndio 'ukaze buti'. Wapo hata wanaume wengine wanasema, hata mimi mke wangu akikubali kuwa kama wewe, niko tayari 'kumsapoti'. Wanaume wanaonidharau ni wachache, wengi wananitia moyo.

"Vijiwe hivi vya dereva Bajaji na bodaboda, kutaniwa ni kawaida, maana kila mtu na akili yake. Yupo mwingine atakutania umezeeka, kakae nyumbani, mara wewe ni wa kuolewa, kwanini unafanya kazi za wanaume? Kikubwa ni kuyapuuza maisha yanaendelea.

### KABEBA ZEGE

"Kikubwa mimi nilichojifunza, mwanamke ukiona hii kazi unaiweza, wewe fanya. Kwa mfano, mimi nimejiamini ninaweza ndio maana niliwahi hata kufanya kazi za kubeba zege Dar es Salaam, Kariakoo. Nilikuwa najitwisha makarai ya zege kipindi hicho sina mbele wala nyuma.

"Kwa hiyo, wanawake wakikariri eti hii kazi ya mwanamume , wasikariri kuwa kazi ya mwanamke ni kusuka nywele na kupika vitumbua. Mbona wapo wanaume wanapika 'mama ntilie' wakati hiyo ndio ilitakiwa kuwa kazi ya mwanamke sasa hivi watu ni kuchangamana.

"Na sisi wanawake kwanza ni waaminifu barabarani na ukishaonekana pia ni rahisi kupata ajira. Mimi nilishaonyesha leseni yangu, watu wananiambia 'Mama Lao ongeza madaraja' sisi tutakupa ajira ya kuendesha magari makubwa," anasema Mama Lao.

### WANAOISHI NAYE

Meshack Fanuel na Mrisho Shabani, ni vijana waajiriwa wa kuendesha Bajaji na mama huyo, nao wana maoni yao.

"Kiukweli nimpongeze mama lao ametujali sisi vijana na kutupa ajira.Nilikuja hapa kijiweni, sikutegemea kama nitakutana na mwanamke ambaye anajua kuendesha Bajaji na sisi sasa hivi tunakula, familia zetu zinaishi kupitia yeye," anatamka Mrisho.

"Mama Lao ni mwanamke ambaye ana upendo na heshima. Nilienda kumueleza shida zangu za kuhitaji kazi ya udereva Bajaji, kwa uaminifu alio nao akanikubali nifanye kazi na yeye.

Meshack anayeunga mkono: "Niwashauri wanawake wengine wajitume kazi ya bajaji ni kazi kama kazi zingine mwanamke yeyote anaweza kufanya mfano huyu na wanawake wengine wawili nimewaona kwenye kazi hii.

### MWENYEKITI WANA – BAJAJI

Rayson Kang'ombe, ni Mwenyekiti wa Chama cha Umoja wa Waendesha Bajaji katika Manispaa ya Mpanda, anasema toka Bajaji ziingie Mpanda mwaka 2013, hakujawahi kutokea mwanamke anaeziendesha.

"Sisi wenyewe hatukujua kama huyu mwanamke ataweza na kuvumilia mpaka leo, toka amekuja huku kwenye udereva bajaji. Yaani amekuwa ni mwanamke wa mfano kwa wanawake wengine wote. Mimi nampongeza ni mwanamke anayejituma, ana pambana, namwambia aendelee kuwa mfano,"anasema Rayson.

# Undani wa mapambano Ofisi Vijana serikalini kuwafungulia fursa za ajira

**Na Magabilo Masambu**

INAJULIKANA hadi sasa kuna tatizo la ajira na maendeleo ya vijana kwa ujumla, nchini na kwingineko duniani. Kila kona vijana wanalalamikia haja kupata maisha bora, serikali nchini na kimataifa zimekuwa zikihangaika kuona tatizo hilo linapungunzwa.

Mnamo katikati ya mwezi uliopita, Nipashe ilikuwa katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Idara ya Vijana, yenye dhamana na maendeleo ya vijana, kudodosa mipango yao katika kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira kwa umma.

Hapo, Ofisa Mkuu wa Maendeleo ya Vijana katikia Ofisi ya Waziri Mkuu, Godfrey Massawe, anaeleza mipango inayotekelezwa ofisini ni kwake, ni kuzama katika upatikanaji wa fursa za ajira nchini nchini kote kukidhi wanayoyataka vijana.

Massawe anataja maeneo muhimu ambayo wizara imejikita katika kuwaimarisha vijana, akinena: "Kwanza tunazo programu zinazowawezesha vijana kujitolea nchini, ili waweze kupata ujuzi bila malipo na kuwafanya waweze kukidhi sifa za kuajirika, kama unavyofahamu ziko kazi zinahitaji uzoefu.

"Pili, ni eneo la ushiriki na ushirikishwaji wa vijana.Tuna programu ambazo tunashirikiana na taasisi mbalimbali, tuna masuala ya kikanda na kimataifa.Tunapozungumzia masuala vijana na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, vijana na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), vijana na AU, vijana na maziwa makuu, vijana na masuala ya ulinzi na amani, kitengo hiki kinasimamiwa na Ofisa Maendeleo ya Vijana"

Masawe anataja programu inayoitwa 'Mama Wadogo' ikiwahusu wasichana waliopata mimba katika umri kati ya miaka 15 na1 9, hapo kwa kushirikiana na serikali za mitaa, wanahakikisha wanalifikia kundi hilo, kuwapatia elimu sahihi ya afya ya uzazi, pia ujasiriamali, kuwezesha kuwaunganisha na fursa zilizopo za kiuchumi, kwa kushirikiana na wadau wanaoweza kubaini mahitaji yao, ili kuwasaidia.

Eneo la tatu, analiorodhesha ni Kitengo cha Ushauri Nasaha, katika utoaji wa elimu ya kujikinga na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi, pia wanaojihusisha na dawa za kulevya, wakipatiwa mafunzo yanayohusu mabadiliko ya tabia chanyaa.

MWENGE NA WABIA WAKE

Kimsingi, shughuli za Mwenge wa Uhuru zinaratibiwa na Idara ya Maendeleo ya Vijana katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Ni shughuli ya kitaifa ukizunguka nchi nzima, katika mikoa 31 yenye jumla ya halmashauri 191.

Ni kawaida, kilele chake huwa ni tarehe 14 Oktoba, siku ya kumbukizi ya kifo cha Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, kipindi ambacho pia ni Wiki ya Vijana, kati ya tarehe 8 na 14.

Ofisa Maendeleo ya Vijana Mwandamizi, Godfrey Chacha, anaeleza vijana wanavyoshirikishwa katika mipango mbalimbali ya maendeleo, akitaja, uchumi jumuishi ukiwashirikisha wote, akitoa mfano wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, akisisitiza,

siyo jukumu la wizara pekee, bali ni ushirika wa pamoja.

"Ni muhimu kufahamu kama vijana wenyewe wanao ujuzi wa kushiriki katika shughuli hizo za maendeleo, ndiyo maana sisi kama Idara ya Vijana na wizara kwa ujumla, tunaandaa mafunzo mbalimbali kuwawezesha vijana kuendana na soko la fursa zinapotokea," anasema.


Chacha, pia anazungumzia suala la kujitolea, akiwa na mtazamo: "Kuna umuhimu sasa wa kuweka programu za vijana wetu kwenda katika mataifa mengine kujitolea, ili wakajifunze ujuzi mbalimbali unaopatikana huko, kisha wanarejea hapa nchini kulinufaisha Taifa.Ni kwa sababu katika programu zetu, tunawafundisha pia wawe wazalendo, maana yake watajifunza kwa manufaa ya nchi."

Amina Sanga, Ofisa Maendeleo ya Vijana Mwandamizi, anaezieleza sera mbalimbali zinazotungwa na kusimamiwa na ofisi hiyo, akifafanua: "Tunayo Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007 ambayo inaeleza mambo mbalimbali kuwahusu vijana.

"Sera hii inaeleza juu ya usawa wa kijinsia katika maendeleo ya vijana, haki za vijana, ushiriki wa vijana katika kilimo na ufugaji, vijana elimu na mafunzo, upatikanaji wa habari, mawasiliano na maarifa, ushiriki wa vijana na utawala bora haya ni machache tu kati ya mengi yaliyoelezwa katika sera hii".

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Kwa madudu haya ya CAG, hatua za wazi zionekane






NA JOSEPH KULANGWA
(+255) 713 410008
kulangwasos@gmail.com

JUZI kati hapa nilisoma habari kwenye mitandao hii ya kijamii, kwamba kuna wananchi katika eneo la jimbo fulani, wanasikitikia miundombinu ya daraja kuzibwa na taka wakati huu wa mvua.

Wananchi hao wakihanikiza kuwa ni kero ya muda mrefu hususan mvua inaponyesha, kwani taka za kila aina huhamia darajani hapo na kuliziba, huku majitaka yakipita juu yake na kuzuia watu kupita.

Unajua tena mambo ya mitandaoni, mwananchi mwingine badala ya kusikitika na wenzake, yeye akaibuka na kumsifu mbunge wake, kwamba amekuwa akijitolea kutengeneza daraja hilo lililoko chini ya TARURA.

Nikajiuliza, kama mbunge amekuwa akijitolea kutengeneza daraja hilo, iweje sasa linaziba na kusababisha kero za aina hiyo? Nikagundua kumbe hakuna ufuatiliaji, ila mbunge alikuwa akipita ili kupata kiki.

Kama kweli angelikuwa anafuatilia miundombinu hiyo, iweje mvua inyeshe taka zizibe daraja? Angekuwa anafuatilia, ina maana kusingekuwapo taka za kuliziba wakati wa mvua. Kufuatilia si darajani, bali kuangalia mitaro ipelekayo maji sehemu hiyo.

Tatizo letu binadamu, tunakimbilia matokeo, badala ya kuangalia chanzo cha matokeo hayo. Tunakimbilia tiba, badala ya kinga dhidi ya maambuki zina madhara yake.

Jambo hili lilikuja wakati nikitafakari hili alilotoa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere katika taarifa yake ya mwaka 2021/22.

Hakika taarifa hiyo ni kama yaleyale aliyoyatoa mwaka jana, ulaji na upigaji uko palepale kana kwamba hakupata kuliambia taifa jinsi uhalifu huu unavyotokea na kuendelea kukita mizizi kwa maslahi finyu ya wananchi.

Inavyoonekana, watu wanapewa dhamana kumsaidia Rais, lakini ndiyo kwanza wanakengeuka na kufanya wanayoona kuwa yanawanufaisha wao na si wananchi waliochangia kuwafikisha hapo walipo.

Wanashindwa kuona jinsi Rais anavyopambana kuiokoa nchi na kuirejesha mstarini katika maendeleo na badala yake, wanamchekelea usoni huku kisogoni wakimng'ong'a.

Hivi kweli wananchi na viongozi tungekuwa kweli tunatenda tunayoyasema na kuyahubiri taka zingeziba madaraja kweli? Barabara zingebomoka? CAG Kichere angeibua madudu kila mwaka wa ukaguzi?

Hii ni awamu ya kwanza ya ukaguzi, tayari tumeshaanikiwa madudu hadharani, tusubiri awamu ya pili itakayofanywa na Mwenge wa Uhuru, ambako nako hakutakosekana madudu yatakayoanikwa na wahusika kuchekelea.

Mtu unakubali dhamana ya kufanya jambo, unaapishwa kwa unyenyekevu, lakini baada ya kuanza kazi unafanya ujuavyo wewe, kwa kuwa tu Rais hawezi kufika kote kwa muda uleule!

Rais akiamua kuwa mkali mtamwita dikteta, akiwa mpole mtasema anacheka cheka, wengine wakisimama kumsaidia aone mengi na kuchukua hatua, mtasema wastaafu wanaweweseka. Yote hiyo ni ili mwendelee kula bila kunawa.

Naamini Tume ya Haki Jinai iliyoundwa na Rais Samia Suluhu Hassan, inaendelea kukusanya maoni ya wananchi kuhusu nini la kufanya hususan kwenye haki, itayaona haya na mengine, hata kuja na mapendekezo.

Hii nchi isipokuwa na viongozi wakali, viongozi wanaojali haki na maslahi ya Watanzania walio wengi kama anavyojitahidi kufanya Rais Samia, tutaiacha mikononi mwa majizi na majambazi tukishuhudia wananchi wa kawaida wakiendelea kuwa wa kawaida na kawaida zaidi na kudidimia.

Endapo hatua hazitachukuliwa kwa hawa walioanikwa na CAG Kichere na kuhakikisha wengine wanaoshuhudia zikichukuliwa, hapatakuwa na sababu ya kuwa na CAG.

Ni dharau kuwa taarifa ya mwaka jana ilitoa madudu kama haya haya ya mwaka huu na zaidi na kama watuhumiwa waliendelea kubaki ofisini kana kwamba nchi hii wameibinafsisha, itafaa tujiulize kulikoni.

Tunaposhindwa kumsaidia Rais kupambana na ubadhirifu na udanganyifu na matokeo yake uchafu huu kujirudia, basi tukubali kuwa hatufai na tujikalie pembeni waje wanaoweza kumsaidia.

Ni aibu kusikia ndani ya jeshi la Polisi, kuna wizi mahali ambako kulipaswa tabia hiyo isiwapo kabisa wala dalili zake. Kwanini jeshi linalopambana na wizi kila kukicha au tunaposikia ofisi za mashitaka nazo hazijakaa sawa, unakuwa mtihani!

UCHUMI

# UTT, yafanikiwa ‘kuchanja’ uwekezaji mtaji kwenye kundi la taifa la kesho

**Na Frank Monyo**




Sehemu ya kada muhimu katika uwekezaji tajwa wa UTT. **PICHA: MTANDAO**

KATIKA miaka karibuni, kumekuwapo mwamko wa Watanzania kujikita kuwekeza aina tofauti tofauti, ikihusisha kupunguza ugumu wa maisha.

Familia nyingi, zimekuwa zikipambana katika kujenga misingi bora kwa watoto kwa kuhakikisha wanapata elimu bora,maisha bora kwa ajili ya kuwaandalia maisha ya baadae.

Kampuni ya UTT AMIS iliyo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango, imekuwa na mchango mkubwa kwa kundi hilo, kuchochea uwekezaji huku wakitoa elimu ya fedha na uwekezaji hasa katika mfuko wake, Watoto Fund.

“UTT AMIS tunatambua umuhimu wa mtoto kwa maendeleo ya taifa katika siku zijazo. Kwa sababu hii ndio maana Mfuko wa Watoto (Watoto Fund) ulizinduliwa.

“Mfuko wa watoto ni suluhisho la kifedha ambalo linalenga katika kukuza mtaji kwa faida ya muda mrefu kwa ajili ya maendeleo ya watoto wetu wapendwa,” Hii ni kauli ya Ofisa Mwandamizi wa Masoko na Uhusiano wa UTT AMIS,” anasema Rahim Mwanga.

Mwanga, anaimbia Nipashe, umuhimu wa wazazi kuwekeza katika Mfuko wa Watoto kwa ajili ya maendeleo ya baadae hasa katika elimu.

Anafafanua kuwa, mfuko huo ni mpango ulio wazi kwa watoto unaokusudia kukuza mtaji kwa muda mrefu kupitia uwekezaji wa mseto, kwa kuwekeza kwenye hisa zilizoorodheshwa kwenye soko la hisa na dhamana.

Anasema umri wa mtoto wa kujiunga na mfuko, uwekezaji unafanywa kwa mtoto wa umri chini ya miaka 18 na anayeruhusiwa kuwekeza: kwa Watanzania walio ndani na nje ya nchi, pia watu binafsi, kampuni, taasisi, benki na asasi za kiraia, huku uwekezaji ukitakuwa ufanywe kwa manufaa ya mtoto.

“Watoto wote wenye umri wa miaka 0 hadi 18 wanaweza kujiunga na mpango huu. Kiasi cha awali kinachohitajika kwa uwekezaji ni shilingi 10,000. Uwekezaji wa ziada ni kuanzia shilingi 5,000na kuendelea ambao unaweza kufanywa kadiri ya mwekezaji awezavyo,” anasema Mwanga.

**USHAURI WAKE**

Mwanga, anatoa ushauri kwa wazazi na walezi kujenga mazoea ya kuweka akiba kwa kufanya uwekezaji na UTT AMIS kwa ajali ya watoto, anasema hii ndio njia pekee itakayowajengea uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya kiuchumi kwa miaka ya mbele na kutoa fursa kwa watoto kupata mahitaji hasa elimu bila pingamizi

**THAMANI YA MFUKO**

Mwanga anasema, thamani ya kipande kwa kipindi cha mwaka mmoja ulioisha tarehe 30 Juni mweaka jana, iliongezeka kufikia shilingi 519.3 kwa kila kipande kutoka shilingi 455.2 , ya Juni 2021, sawa na ukuaji wa asilimia 14.1 kwa mwaka.

Anasema, inaonyesha ukubwa wa mfuko kuongezeka kwa asilimia 35.7 (shilingi bilioni 1.5) kutoka shilingi bilioni 4.2 hadi kufikia shilingi bilioni 5.7.

Anafafanua kuwa, katika kipindi cha mwaka wa fedha ulioisha tarehe 30 mnamo Juni mwaka jana, Meneja wa Mfuko alitumia uzoefu kufikia mgawanyo anuai wa rasilimali kwa mujibu wa matakwa ya Sera za MKfuko wa Watoto.

Anataja dhamana za muda mrefu zilichukua sehemu kubwa, asilimia 73.1, ikifuatiwa na asilimia 24.2, na amana za benki za muda mfupi, asilimia 2.7.

**FAIDA ZILOZOKO**

Anasema kuwa faida katika mfuko wa Watoto kwa mwaka wa fedha ulioisha Juni 2022 ilikuwa ni asilimia 14.1 ikilinganishwa na asilimia 19.9 ya mwaka 2021. Kupungua kwa faida ya mwaka kulichangiwa na kushuka kwa viwango vya riba sokoni kama inavyoonekana kwenye Jedwali namba II & V.

“Hali ya utendaji wa mfuko inaonekana ni nzuri na shindani ikilinganishwa na kigezo cha ufanisi na maeneo linganifu, ambapo kwa mwaka 2022 faida ni asilimia 14.1 ikilinganishwa na asilimia 8.7,” anasema Mwanga.

**MWENYEKITI UTT**

Mwenyekiti wa Bodi ya UTT AMIS, Casmir Kyuki, anasema matarajio ya mwaka 2022/23 ya utekelezaji wa mpango mkakati wa UTT AMIS utakaoishia Juni 30, 2024, umekuwa na mafanikio makubwa zaidi ya ilivyotarajiwa.

Anataja mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kulinganisha faida za uwekezaji katika Mfuko wa Watoto kuwa ni; Viwango vya riba kabla ya kutoa kodi ya zuio (withholding tax) ya asilimia 10 wakati faida ya mfuko wa Watoto ni baada ya kutoa kodi ya zuio ya asilimia 10.

“Jambo lingine la muhimu la kuzingatia ni kwamba mfuko wa Watoto unaruhusu wanachama wake kuuza vipande vyao wakati wowote hivyo kumpa fursa mwekezaji kupata fedha pindi anapozihitaji na kwamba hakuna kiwango cha chini cha uwekezaji kinachoruhusu kupata faida,” anasema na kuongeza;

“Viwango vya faida kwenye mfuko vinatolewa sawa kwa wawekezaji wote (wawekezaji wa kipato kidogo, wa kipato cha kati na wale wenye kipato kikubwa),”.

Anasisitiza kuwa kuwekeza kwenye mfuko wa Watoto kuna faida zaidi ya kuwa na akaunti ya amana kwa sababu inamuongezea mwekezaji kipato kikubwa kutokana na viwango bora vinavyotolewa na mfuko zaidi ya viwango vya amana vilivyopo kwenye soko la fedha.

**KUONGEZA WAWEKEZAJI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Uwekezaji ya UTT AMIS, Simion Migangala, wakati wa mkutano wa mwaka uliofanyika Novemba 2022 alisema taasisi hiyo kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2022 imeendelea kufanya vizuri katika mifuko yake yote.

> **Pamoja na changamoto mbalimbali ambazo Dunia inakabiliana nazo, uchumi wa Tanzania uliendelea kufanya vizuri na kuhimili mtikisiko hasa uliosababishwa na matatizo ya vita nchini Ukraine.**

Hapo anataja Mfuko wa Umoja, thamani yake ikiongezke mfuko ikiwa imeongezeka kutoka Shilingi bilioni 612.8 kwa Juni 30, 2021 hadi kufikia Shilingi bilioni 996.5 kwa Juni 30, 2mweaka jana, sawa na asilimia 12.

Ongezeko hilo la kiasi cha Shilingi bilioni 383.7 ni sawa na asilimia 62.6 ikilinganishwa na ongezeko la Shilingi bilioni 206.8 sawa na asilimia 50.0 kwa mwaka uliotangulia.

Anayataja ni mafanikio ya kwanza,a tangu kuanzishwa kwa UTT AMIS na mifuko yake ambapo inashuhudia ongezeko kubwa kama hilo ndani ya kipindi cha mwaka mmoja.

Ongezeko la ukubwa wa mifuko hiyo umeenda sambamba na ongezeko la idadi ya wawekezaji 29,832 sawa na asilimia 17.0 waliojiunga katika mifuko kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30,2022 ikilinganishwa na wawekezaji 12,798 sawa na asilimia 8.0 waliojiunga katika mwaka wa fedha uliotangulia.

“Kama nilivyosema hapo awali, mifuko yote imetoa faida nzuri kwa wawekezaji wake. Faida kwa Mfuko wa Umoja ilikuwa asilimia 12.6. ikilinganishwa na asilimia 8.7 ya Kigezo Linganifu.

“Katika kipindi cha mwaka wa fedha ulioishia Juni 2022, thamani ya Mfuko iliongezeka kutoka Shilingi bilioni 258.0 iliyofikiwa tarehe 30 Juni 2021 hadi Shilingi bilioni 289.0 tarehe 30 Juni 2022. Ongezeko hili la thamani ya Mfuko linatokana na imani ya Wawekezaji pamoja na kuelewekа kwa elimu inayotolewa kuhusu faida za mifuko ya uwekezaji wa pamoja,” anatamka Migangala na kuongeza kuwa:

“Pamoja na changamoto mbalimbali ambazo Dunia inakabiliana nazo, uchumi wa Tanzania uliendelea kufanya vizuri na kuhimili mtikisiko hasa uliosababishwa na matatizo ya vita nchini Ukraine.

“Kwa mujibu wa machapisho ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Pato la Taifa lilikua kwa asilimia 5.4 katika kipindi cha robo mwaka kilichoishia tarehe 31 Machi 2022 na asilimia 4.8 kwa robo mwaka iliyoishia tarehe 30 Juni 2022, ikilinganishwa na asilimia 4.9 na aslimia 4.3 za robo ya tatu na ya nne za mwaka wa fedha 2020/2021.

“ Ripoti ya Benki Kuu ya robo mwaka iliyoishia tarehe 30 Juni 2022, inasema mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 4.1 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 9.4 katika nchi za Afrika Mashariki na wastani wa asilimia 10.1 kwa nchi za ukanda wa SADC ukiondoa nchi ya Zimbabwe,” alisema.

# LETSHEGO BANK (T) LIMITED

Letshego Bank

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA

### IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.12.2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| (Kiasi kwa shilingi '000) | | 31-Esfand-22 Iliyokaguliwa | 31-Esfand-21 Iliyokaguliwa |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 785 | 845 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 598 | 1,146 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 8,010 | 4,790 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | 51 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa Kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 13,460 | 20,677 |
| 12 | Mali Nyingine | 10,631 | 2,237 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za Udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,246 | 1,340 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | 34,730 | 31,086 |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 1,701 | 2,437 |
| 18 | Amana za Wateja | 7,946 | 7,858 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa fedha Tslimu | 0 | 0 |
| 20 | Amana Maalumu | 0 | 0 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za kuhamisha | 0 | 0 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 0 | 0 |
| 23 | Limibikizo za Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 0 | 0 |
| 24 | Dhima la Tozo Kwaajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Meneja | 0 | 0 |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo | 0 | 0 |
| 27 | Dhima Nyingine | 1,412 | 834 |
| 28 | Madeni | 1,242 | 5,308 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **12,300** | **16,438** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 KUTOA 20)** | **22,429** | **14,648** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 53,489 | 47,831 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 783 | 105 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (33,966) | (28,307) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 2,124 | (4,981) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 0 | 0 |
| 36 | Stahiki ya wenye Hisa Chache | 0 | 0 |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **22,429** | **14,648** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | - | - |
| 39 | Mikopo chechefu (Zaidi ya Siku 30) | 8,573 | 6,686 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 6,564 | 4,937 |
| 41 | Mali nyingine chechefu | - | - |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 65% | 47% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 43% | 26% |
| | | 0% | 0% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 208% | 249% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 39% | 67% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 62% | 92% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -6% | 26% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 12% | -20% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA INAYOISHIA 31.12.2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| (Kiasi kwa shilingi '000) | | 31-Desemba-22 Iliyokaguliwa | 31-Desemba-21 Iliyokaguliwa |
|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 3,182 | 5,532 |
| 2 | Gharama za Riba | (1,172) | (1,364) |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2) | 2,009 | 4,168 |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | (21) | (722) |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la Tengo katika Mikopo | (1,397) | (338) |
| 6 | **Mapato yasiyo na Riba** | 506 | 406 |
| | 6.1 Faida/(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya | - | (6) |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 506 | 394 |
| | 6.3 Gawio | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | - | 19 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba** | (6,874) | (8,465) |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (3,091) | (3,728) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - |
| | 7.3 Gharama nyingine | (3,783) | (4,737) |
| 8 | **Faida / (Hasara) ya Uendeshaji** | (5,777) | (4,952) |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 7,900 | (30) |
| 10 | **Faida / (Hasara) Hasili Baada ya Kodi ya Mapato** | 2,124 | (4,981) |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumulisha (bainisha) | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa** | 2,124 | (4,981) |
| 13 | **Idadi ya Waajiriwa** | 76 | 71 |
| 12 | Mapato kwa Hisa | 0 | (0) |
| 13 | Mapato ya Hisa zilizochujwa | 0 | (0) |
| 14 | **Idadi ya Matawi** | 5 | 5 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 6% | -14% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa fedha za wanahisa | 6% | -34% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | -261% | -172% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazo Zalisha | 17% | 17% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31.12.2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| Kisia kwa Milion | | 31-Desemba-22 Audited | 31-Desemba-21 Audited |
|---|---|---|---|
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (5,777) | (4,952) |
| I: | **Marekebisho Kwa Ajili ya** | - | |
| | -Uchakavu katika Mikopo | 1,418 | 1,061 |
| | -Uchakavu katika Mali | 913 | 933 |
| | -Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya mali | 125 | (7) |
| | -Hasara katika Mali | - | - |
| | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za uwekezaji;** | **(3,322)** | **(2,965)** |
| | -Badiliko Halisi katika Mikopo | 7,217 | 6,607 |
| | -Faida/Hasara katika mauzo ya mali | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi katika Amana | (1,352) | (3,682) |
| | -Mabadiliko Halisi katika mali nyingine | - | - |
| | -Mabadiliko halisi katika Dhima nyingine | - | - |
| | -Mabadiliko ya kiwango kinachoitajika na Bank kuu ya Kisheria | 114 | 148 |
| | -Mabadiliko Halisi katika Mikopo | 135 | (256) |
| | -Mabadiliko Halisi katika Amana | (447) | (437) |
| | -Kodi iliyolipwa | (28) | (30) |
| | -Mengineyo/(Bainisha) | (196) | (112) |
| II. | **Jumla ya Fedha kutokana na Shughuli za uwekezaji** | **2,120** | **(727)** |
| | **Mtiririko wa Fedha kutokana na shughuli za uwekezaji** | | |
| | Gawio lililopokewa | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za kudumu | (26) | (71) |
| | Mapato kutokana na mauzo ya Mali za Kudumu | - | 7 |
| | Ununuzi wa amana zinazoshugulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Ununuzi wa ama zisizoshugulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Fedha Halisi zilizotolewa/(zilizotumika) kwa shughuli za Uwekezaji | - | (164) |
| III. | **Jumla ya Fedha kutokana na Shuguli za uwekezaji** | **(26)** | **(229)** |
| | **Mtiririko wa Fedha kutokana na shughuli za kifedha** | | |
| | Ulipaji wa madeni ya mda mrefu | (4,568) | (1,503) |
| | Mapato Kutokana na mikopo ya Kudumu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Hisa | 5,658 | 2,824 |
| | Gawio lililolipwa kwa Fedha Taslim | - | - |
| | Mengineyo/(Bainisha) | - | - |
| | Mabadiliko halisi katika madeni Mengine | (492) | (456) |
| IV. | **Jumla ya Fedha kutokana na shughuli za Kifedha** | **597** | **865** |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu kwa Mwaka** | | |
| | **Mabadiliko halisi ya Fedha na mali zinazofanana na Fedha taslimu** | **2,691** | **(91)** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu mwanzoni mwa Mwaka. | **6,157** | **6,248** |
| | **Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwishoni mwa Mwaka.** | **8,848** | **6,157** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA MWAKA ULIOISHIA 31.12.2022

| Mwaka wa Sasa 2022 | | Mtaji wa Hisa | Mtaji utokanao na hisa za upendeleo | Ziada ya Kisheria | Hasara Kusanyiko | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | | **39,311** | **8,520** | **105** | **(33,288)** | **14,648** |
| 1 | Mapatao mengine yaliyojumuishwa | 5,658 | - | - | - | 5,658 |
| 2 | Tengo la ziada ya Jumla | - | - | 678 | (678) | - |
| 3 | Ziada Ya Kisheria | - | - | - | - | - |
| 4 | Mengineyo - ( IFRS -9) | - | - | - | | - |
| 5 | Faida /(Hasara) baada ya kodi ya mapatao | - | - | - | 2,124 | 2,124 |
| 6 | Mengineyo | - | - | - | - | - |
| 7 | | | | | | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | | **44,969** | **8,520** | **783** | **(31,843)** | **22,429** |
| **Mwaka Uliopita 2021** | | | | | | |
| **Salio la Mwanzo wa Mwaka** | | 36,487 | 8,520 | 0 | (28,202) | 16,805 |
| 1 | Mapatao mengine yaliyojumuishwa | 2,824 | - | - | - | 2,824 |
| 2 | Transfer to general Provision reserve | - | - | 105 | (105) | - |
| 3 | Tengo la ziada ya Jumla | - | - | - | - | - |
| 4 | Ziada Ya Kisheria | - | - | - | - | - |
| 5 | Faida /(Hasara) baada ya kodi ya mapatao | - | - | - | (4,981) | (4,981) |
| 6 | Mengineyo | - | - | - | - | - |
| 7 | | - | - | - | - | - |
| **Salio la Mwisho wa Mwaka** | | **39,311** | **8,520** | **105** | **(33,288)** | **14,648** |

Signed by:

**Omar S. Msangi**
(Mkurugenzi Mtendaji)

**Rashid Sendoro**
(Mkaguzi wa ndani)

**Isaack Chahe**
(Meneja wa Fedha na Utawala)

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uendeshaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikuwa na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha mwaka sasa,

**Simon Jengo**
(Mwenyekiti wa Bodi)

**Noel Sangiwa**
(Mkurugenzi)

Sisi, tuliotajwa hapo juu, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benk na Taasisi za Fedha ya Mwaka 2006, nazinaonesha hali halisi.





# CRB yawafutia usajili makandarasi 500

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

BODI ya Usajili wa Makandarasi nchini (CRB), imefuta usajili kwa makandarasi 500 baada ya kubaini kutojihusisha na kazi hiyo.

Kwa mujibu wa Msajili wa Bodi hiyo, Mhandisi Rhoben Nkori jana alisema makandarasi hao walifutiwa usajili huo mwaka 2022 baada ya kufanya uchambuzi wa makandarasi na kubaini kutojihusisha kikamilifu na shughuli kwa muda mrefu.

Alisema lengo la kuchukua hatua hiyo ni kujenga imani kwa serikali na bodi kuhusu utendaji kazi katika kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi ya miundombinu yakiwemo majengo, barabara na madaraja.

"Kwa mwaka 2022 bodi ilisajili makandarasi 1,341 na kufanya idadi ya waliosajiliwa kufikia 14,034, idadi ya usajili imeongezeka kwa wastani wa 900 kwa mwaka," alisema Mhandisi Nkori.

Aliongeza kuwa bodi iliendesha kozi tano za mafunzo kwa makandarasi kwa madhumuni ya kuwajengea uwezo kwenye maeneo mbalimbali na kwamba miradi 4,013 yenye thamani ya Sh. trilioni 6.1 ilisajiliwa.

Aliikumbusha serikali kuongeza kiwango cha malipo ya awali sambamba na nyongeza ya kiwango cha malipo kutoka asilimia 15 ya sasa hadi 25 au zaidi kulingana na mahitaji halisi ya mradi husika.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya, alisema kuna uhaba wa mitambo ya ujenzi wa miundombinu hususani barabara.

Alisema kukosekana mitambo ya kujengea barabara imesababisha kuchelewa kukamilika kwa miradi mingi inayojengwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

"Miradi mikubwa ya ujenzi wanapewa zaidi wageni kuliko wazawa kutokana na kukosa wataalamu wabobezi wa ujenzi lakini pia kukosa mitambo ya kisasa kwa ajili ya kuitekeleza," alisema Mhandisi Kasekenya.

Aidha aliagiza bodi ya makandarasi kudhibiti wimbi la makandarasi wasiokuwa waaminifu ambao hawakamilishi miradi kwa wakati na kutozingatia ubora unaoendana na thamani ya fedha zilizotolewa.

Alisema kufanya hivyo kunakwamisha jitihada za serikali katika kuwaletea maendeleo wananchi kutokana na uzembe wa baadhi ya makandarasi.

Miongoni mwa makandarasi walioshiriki mkutano wa mashauriano na wadau wa sekta ya ujenzi, Magdalena Kagwanga aliiomba serikali kutoa ruzuku za ununuzi wa mitambo mikubwa ili kukamilisha miradi ya ujenzi.

Alisema kwa sasa wanashindwa kuikamilisha kutokana na kukosa vifaa vya ujenzi ambavyo vingesaidia miradi kuwa bora ukilinganisha na ilivyo sasa ambapo wanashindwa kupata tenda kutokana na tatizo hilo.

Baraka Ulimboka kutoka Mkoa wa Rukwa alikiri baadhi ya makandarasi kutokuwa waaminifu katika ujenzi wa miradi kwa maana ya kujenga chini ya kiwango na wakati mwingine kutokamilisha kwa wakati.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Afrika Tanzania, Adam Mihayo (kushoto), akizungumza wakati wa futari iliyoandaliwa na benki hiyo kwa wateja wake, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wenye matatizo ya macho Mbarali kutibiwa bure

**Na Grace Mwakalinga,**
MBARALI

SHIRIKA la Hellen Keller International kwa kushirikiana na Wizara ya Afya wanatarajia kutoa huduma ya matibabu kwa wananchi wenye matatizo ya macho wilayani Mbarali.

Kaimu Meneja wa Mpango wa Taifa wa Huduma za Macho kutoka Wizara ya Afya, Dk. Greater Mande, alitoa kauli hiyo wilayani Mbarali ambapo wameweka kambi inayoendeshwa na Wizara ya Afya kupitia watoa huduma wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mbeya kwa kushirikiana na Shirika la Hellen Keller International.

Alisema mradi huu wa upasuaji wa mtoto wa jicho utatekelezwa kwa kipindi cha mwaka mmoja na kwamba wagonjwa watakaobainika watapatiwa matibabu ikiwamo dawa na upasuaji.

"Wizara ya Afya kwa kushirikiana na wadau wetu wa Shirika la Hellen Keller International tumepiga kambi wilayani Mbarali kwa ajili ya kutoa huduma za matibabu ya macho, nawasihi wakazi wa Mbarali kujitokeza kwa wingi kupata huduma hiyo bure," alisema Dk. Mande Alisema shirika hilo linatumia huduma tembezi ya kuwaibua wagonjwa kupita nyumba kwa nyumba kwa hatua ya awali na baadae kuwafikisha kwenye kituo cha kutolea huduma kwa ajili ya upasuaji.

Miongoni mwa vipaumbele vya Wizara ya Afya ni kuwafikia wananchi wenye matatizo ya macho ambao wanaishi maeneo ya pembezoni kupitia huduma tembezi .

Meneja Mradi wa Shirika la Hellen Keller International, Athuman Tawakal alisema kambi hiyo ni ya kwanza wilayani Mbarali na wanatarajia kuwafikia wananchi takribani 900 kutoka maeneo mbalimbali.

Tawakal alipongeza serikali kuboresha miundombinu katika hospitali za wilaya ikiwamo eneo la upasuaji na hivyo kurahisisha huduma za upasuaji kufanyika kwenye wilaya.

Mkazi wa Kijiji cha Muungano, Victoria Mronji, alisema anasumbuliwa na tatizo la mtoto wa jicho kwa muda mrefu na kumsababishia kutokuona, hivyo anaamini uwepo kwa kliniki hiyo itamsaidia kupata matibabu sahihi na kupona ugonjwa unaomsibu.

# Wananchi walia kupanda bei gesi ya kupikia

**Na Grare Mwakalinga,**
MBEYA

WANANCHI mkoani Mbeya wameiomba serikali kupunguza gharama za upatikanaji wa gesi safi kutokana na wananchi wengi kushindwa kumudu gharama, hali inayochangia kuendelea kwa matumizi ya nishati zinazoathiri mazingira.

Triphonia Kabende kutoka Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, (MUST) alisema pamoja serikali kuhamasisha wananchi kutumia nishati mbadala kwa lengo la kutunza mazingira, jitihada hizo zinapaswa kwenda sambamba na kupunguza gharama kubwa za upatikanaji wa gesi nchini ili kuwafikia wananchi wa kipato cha chini.

"Tumesikia serikali inakuja na mpango wa matumizi ya mabomba ya gesi lakini hadi sasa wananchi hawajui itakuaje ukilinganisha na ile ya kuweka kwenye mitungi, nashauri elimu itolewe lakini waangalie na gharama zake kwa wananchi kwa sababu gesi inauzwa kwa gharama ambayo wananchi wengi wa kipato cha chini hawawezi kumudu,"alisema Trifonia.

Benard Mwakasitu alisema kumukuwepo na uharibifu mkubwa wa mazingira kutokana na matumizi ya nishati isiyo safi hasa kuni na mkaa ambazo matokeo yake ni ukataji miti, hivyo serikali inapaswa kuweka mikakati itakayowezesha upatikanaji wa nishati mbadala kwa bei nafuu ili wananchi waachane na matumizi ya nishati zinazoharibu mazingira.

Hivi karibuni, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ushindani (FCC), Zaytun Kikula akiwa mkoani Mbeya, alisema vikwazo wanavyokabiliana navyo watumiaji wa nishati safi ni gharama kubwa za upatikanaji wa nishati hizo ambapo wananchi wengi hawawezi kumudu.

# Majaliwa kuzindua machapisho ya Sensa ya Watu na Makazi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Tanzania Bara na Zanzibar zinatarajia kuzindua machapisho ya taarifa za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, Aprili 15 mwaka huu visiwani Zanzibar.

Uzinduzi huo utazinduliwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati Kuu ya Taifa ya Sensa ya Watu na Makazi.

Akizungumza na waandishi wa Habari, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera na Uratibu wa Shughuli za Baraza la Wawakilishi, Hamza Hassan Juma, alisema tukio hilo ni muhimu na msingi mkuu wa upangaji wa utekelezaji wa maendeleo kwa maslahi ya taifa.

Alisema machapisho mawili makuu yatazinduliwa ikiwamo la mgawanyo wa maendeleo ya watu kwa maeneo ya utawala na chapisho la mgawanyo wa watu kwa umri na jinsia.

"Machapisho hayo taarifa zake zimetolewa na kugawanywa katika makundi matatu ambayo ni taarifa za Tanzania kwa jumla, Tanzania Bara na Zanzibar,"alisema Hamza.

Alisema hatua hiyo ni muhimu ambayo ni mafanikio makubwa kwa wataalamu waliofanya kazi kwa umakini mkubwa kwa kuzikusanya na kuzichakata taarifa hizo na kuwa takwimu bora na sahihi kwa matumizi ya wadau mbalimbali katika sekta ya elimu na maendeleo.

Aidha, alisema umuhimu mkubwa wa takwimu zilizopatikana katika sensa ya watu na makazi ni pamoja na kutumiwa katika kutunga sera, mipango ya bajeti kwa kila sekta kwa lengo la kupanga mipango ya maendeleo.

"Matumizi ya takwimu ya Sensa ya Watu na Makazi yatasaidia sana katika usambazaji na uimarishaji wa huduma za mbalimbali za kiuchumi na kijamii, biashara na uwekezaji," alisema.

Hamza alisema kuna wajibu wa kuhakikisha kuwa na takwimu za sensa kama dira na mwongozo katika kuongoza serikali vyema katika utekelezaji wa mahitaji ya msingi kwa wananchi.

Alisema takwimu hizo pia zitatumika kuwezesha na kutunga, kufanya mapito ya sera ya mipango ya maendeo ya utawala na kufanya chambuzi za kitaalamu katika nyanja mbalimbali za kufanya maamuzi ambazo zitawezesha sera za kijamii na kiuchumi kuwa endelevu na zinazoboresha ustawi wa watu.



Rais wa Zanzibar, Alhaji Dk. Hussein Ali Mwinyi akikabidhi sadaka kwa watu wenye mahitaji maalumu wakiwemo wenye ulemavu, wazee, yatima na wajane, wilayani Chakechake, Mkoa wa Kusini Pemba jana. **PICHA: IKULU**

# Watu 12 wafariki dunia kwa ajali mwezi uliopita

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WATU 12 wamefariki dunia visiwani Zanzibar kutokana na ajali za barabarani katika kipindi cha Machi mwaka huu.

Mkuu wa Divisheni ya Takwimu za Jinsia na Ajira kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, Sabiha Raphael Daima, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wahabari.

Alisema makosa ya barabarani kwa mwezi uliopita yameongezeka kwa asilimia 34.4 kutoka asilimia 30.6 kipindi cha Februari.

Alisema jumla ya makosa 3,064 yameripotiwa kipindi cha Machi mwaka huu ambapo makosa 3,057 yamefanywa na wanaume na makosa saba yamefanywa na wanawake.

Alisema Wilaya ya Kaskazini B Unguja ina idadi kubwa ya makosa ya barabarani ambayo ni 580 kati ya makosa yote yaliyoripotiwa na Wilaya ya Micheweni Pemba ni wilaya yenye makosa kidogo ambayo ni 31.

"Wilaya za Mkoa wa Kaskazini Unguja zimechangia asilimia 33.6 ya makosa yote yaliyoripotiwa, hivyo mkoa huo unaongoza kwa makosa ya barabarani kuwa na makosa 1,030 ikifuatiwa na wilaya za Mkoa wa Mjini Magharib Unguja ambazo zina makosa 1,026,"alisema Daima.

Aidha, alisema idadi ya aina ya makosa hayo kwa mwezi huo kosa kuu ni kutokufuata miongozo na kanuni za usalama barabarani yakifuatiwa na madereva kuendesha chombo cha moto bila ya lesseni.

Alisema sababu za ajali nyingi za barabrani ni mwendo kasi wa baadhi ya madereva pamoja na uzembe wa madereva hao.

Akizungumzia kuhusu utekelezaji wa sheria ya adhabu ya hapo kwa hapo kwa madereva wanaokiuka sheria za barabarani, Sajeti Ali Abdullah kutoka kitengo cha usalama wa barabarani Jeshi la Polisi alisema adhabu hiyo imepunguza msongamano mkubwa wa kesi mahakamani.

"Lengo siyo kwamba watu walipe faini bali lengo ni kutokuwepo kwa makosa ya ajali za barabarani ili kunusuru vifo na ajali zinazoepukika," alisema Sajeti Ali.

# Wanafunzi, wasomi watakiwa kusoma vitabu vya kichina

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, imewataka wadau mbalimbali wakiwemo wanafunzi vijana na wasomi kuitumia maktaba kwa ajili ya kusoma vitabu vikiwemo vya lugha ya kichina.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Ali Abdulgulam Hussein aliyasema hayo jana wakati akipokea msaada wa vitabu vilivyotolewa na Serikali ya China pamoja na kusaini hati ya ushirikiano wa kuisaidia maktaba.

Alisema ikiwa makundi hayo yakitumia vitabu hivyo vilivyotolewa na China anaamini watapata kujifunza mambo mbalimbali ya nchi hiyo ikiwemo sera wanazozitumia na utamaduni wao.

Naibu Waziri huyo alisema Serikali ya China imekuwa rafiki mkubwa kwa Tanzania na Zanzibar na ipo mstari wa mbele katika kusaidia Zanzibar katika nyanja mbalimbali ikiwemo sekta ya elimu.

"Kupitia vitabu hivi tunaamini tutaweza kujifunza masuala mbalimbali yanayohusu utamaduni wa ndugu zetu wa China ambao tumetoka nao mbali," alisema.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Khamis Abdalla, alisema katika sayansi na teknolojia ya karne ya 21 ni lazima mtu awe anajua lugha mbalimbali na lugha inasaidia kwenye mawasiliano na biashara.

Alisema lugha ya kichina ni muhimu na tayari inazungumzwa na asilimia kubwa ya wananchi duniani, hivyo vitabu hivyo vinatoa msingi wa kujifunza lugha ya kichina.

Naye Balozi Mdogo wa China Zanzibar, Zhang Zhisheng, alisema vitabu hivyo vitasaidia wanafunzi kujifunza lugha ya kichina na mambo ambayo ni muhimu.

Alisema urafiki wa China na Zanzibar ni wa muda mrefu baada ya mapinduzi ya mwaka 1964, kwamba vitabu hivyo ni kuendeleza mashirikiano ya zamani yaliyokuwepo baina ya nchi hizo mbili.

# KILIMANJARO CO-OPERATIVE BANK LIMITED

Together, Transforming Lives

## UONYESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DISEMBA 2022
(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| | | Current Year 31st Dec 2022 | Previous Year 31st Dec 2021 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 122,303 | 140,497 |
| 2 | Salio katika benki kuu ya Tanzania | 480,936 | 607,886 |
| 3 | Uwekezaji katika amana za serikali | - | - |
| 4 | Salio katika benki nyingine na Taasisi za fedha | 662,153 | 580,651 |
| 5 | Hundi na miamala ya kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala baina ya matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizofikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za wateja zilizokubalilka | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa benki nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji katika amana nyingine | 2,095,949 | 2,006,543 |
| 11 | Mikopo halisi iliyopo | 7,493,647 | 4,637,985 |
| 12 | Mali nyingine | 337,138 | 254,474 |
| 13 | Uwekezaji wa hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali zisizohamishika,mitambo na vifaa | 366,706 | 242,919 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **11,558,831** | **8,470,955** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za benki nyingine na Taasisi za fedha | - | - |
| 18 | Amana za wateja | 5,923,744 | 5,426,971 |
| 19 | Dhamana ya malipo kwa fedha taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalum | - | - |
| 21 | Maagizo ya malipo /Fedha kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za kibenki zilizotolewa | - | 293 |
| 23 | limbiko la kodi na ghalama zitakazolipwa | - | 27,277 |
| 24 | Dhima la tozo kwaajili ya usuluhishi baina ya benki na mteja | - | - |
| 25 | Fedha za washirika | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya kipindi kijacho na tozo nyingine zitakazo lipwa baadaye | - | - |
| 27 | Dhima nyingine | 1,233,997 | 268,747 |
| 28 | Madeni | - | - |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **7,157,741** | **5,723,288** |
| 30 | **MALMI /(DHIMA) HALISI(16 kutoa 29)** | **4,401,090** | **2,747,667** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa hisa uliolipwa | 15,305,153 | 13,978,990 |
| 32 | Akiba ya mtaji | (65,457) | 26,581 |
| 33 | Mapato yaliyobakizwa | (11,165,866) | (11,551,455) |
| 34 | Faida(hasara)ya kipindi husika | 327,260 | 293,551 |
| 35 | Akaunti nyingine za mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki za wenye hisa chache | - | - |
| 37 | **JUIMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **4,401,090** | **2,747,667** |
| 38 | Dhima zisizo dhahiri | - | - |
| 39 | Mikopo chechefu | 166,808 | 167,103 |
| 40 | Mikopo chechefu | 72,945 | 74,732 |
| 41 | Jumla ya Mikopo ghafi | 7,566,592 | 4,743,668 |
| 42 | Mali nyingine chechefu | | |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa fedha za wanahisa na jumla ya mali | 38.08% | 32.44% |
| (ii) | Uwiano wa mikopo chechefu na jumla ya mikopo ghafi | 2.20% | 3.52% |
| (iii) | Uwiano wa mikopo ghafi na jumla ya amana | 127.73% | 87.41% |
| (iv) | Uwiano wa mikopo halisi na jumla ya mali halisi | 64.83% | 54.75% |
| (v) | Uwiano wa mali zinazozalisha na jumla ya mali | 65.05% | 55.51% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 9.15% | 0.00% |
| (vii) | Ongezeko la mali | 36.45% | 0.00% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI INAYOISHIA 31 DISEMBA 2022
(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| | | Current Year 31st Dec 2022 | PreviousYear 31st Dec 2021 |
|---|---|---|---|
| 1 | Mapato yariba | 937,564 | 551,613 |
| 2 | Gharama za riba | 47,025 | 49,695 |
| 3 | Mapato halisi ya riba(1 kutoa 2) | **890,539** | **501,918** |
| 4 | Madeni viza yaliyopitwa | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (1,787) | (6,025) |
| **6** | **Mapato yasiyo ya riba** | **694,658** | **711,766** |
| | 6.1 Faida/(hasara) zitokanazo na miamala ya fedha za kigeni | - | - |
| | 6.2 Ada na kamisheni | 309,531 | 264,372 |
| | 6.3 Gawio | | |
| | 6.4 Mapato mengine | 385,127 | 447,394 |
| **7** | **Gharama zisizo na riba** | **1,217,369** | **901,664** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 503,285 | 438,414 |
| | 7.2 Ada na kamishani | - | 53,811 |
| | 7.3 Gharama nyingine | 714,084 | 409,439 |
| **8** | **Faida/(Hasara) ya uendeshaji** | **369,615** | **318,045** |
| **9** | **Tengo la kodi ya mapato** | **42,355** | **24,494** |
| **10** | **Faida /(Hasara)Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **327,260** | **293,551** |
| **11** | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa(bainisiha)** | | |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | | |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 22 | 23 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 0 | 0 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 2.83% | 3.47% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 7.44% | 10.68% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 74.47% | 70.89% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 11.77% | 10.58% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA ULIOISHIA 31 DISEMBA 2022
(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| | | Current year 31st Dec 2022 | Previous year 31st Dec 2021 |
|---|---|---|---|
| **I:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 369,614 | 318,046 |
| | **Marekebisho Kwa Ajili ya:** | | - |
| | - Badiliko katika mali isiyoshikika | 38,752 | 18,898 |
| | - Hasara Katika Mali | - | |
| | - Badiliko halisi katika Mikopo | 66,245 | 73,201 |
| | - Faida/Hasara kwenye mauzo ya mali | (2,855,662) | (4,317,292) |
| | - Mabadiliko halisi katika amana | - | - |
| | - Mabadiliko halisi katika amana za muda mfupi zilizo afikiwa | 496,480 | 80,519 |
| | - Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | - | - |
| | - Mabadiliko halisi katika mali nyingine | 956,093 | (646,135) |
| | - Kodi iliyolipwa | (255,245) | (30,267) |
| | - Mengineyo(bainisha) | (93,119) | (489,787) |
| | - Maslahi ya wachache | | |
| | - Madeni na benki nyingine | (89,406) | (17,480) |
| | ***Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika)kwa shughuli za uendeshaji*** | **(1,366,248)** | **(5,010,297)** |
| **II:** | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji:** | | |
| | gawio lililopokelewa | - | - |
| | Ununuzi wa mali za kudumu | (8,144) | (28,440) |
| | Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa amana zisizoshughulikiwa na mawakala | - | - |
| | Mapato kutokana na mauzo ya amana zisizoshughulikiwa na mawakala | - | - |
| | Mengineyo (Bainisha) | (15,414) | (205,159) |
| | ***Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uwekezaji*** | **(23,558)** | **(233,599)** |
| **III:** | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kifedha** | | |
| | Ulipaji wa madeni ya muda mrefu | - | - |
| | Mapato kutokana na utoaji wa madeni ya muda mrefu | - | - |
| | Mapato kutokana na utoaji wa mtaji wa hisa | 1,326,163 | 217,328 |
| | Gawio lilololipwa kwa fedha taslimu | - | - |
| | Mabadiliko halisi katika madeni mengine | - | - |
| | Mengnineyo | | - |
| | ***Fedha halisi zilizotolewa(Zilizotumika) kwa shughuli za kifedha*** | **1,326,163** | **217,328** |
| **IV:** | **Fedha taslimu na mali zinazo fanana na fedha taslimu:** | | |
| | **Ongezeko/Punguzo halisi kaitka fedha taslimu na mali** | **(63,643)** | **(5,026,568)** |
| | **Fedha na mali zinazofanana na fedha taslimu mwanzoni mwa robo ya mwaka.** | **1,329,034** | **6,355,603** |
| | **Fedha na mali zinazofanana na fedha taslimu mwishoni mwa robo ya mwaka.** | **1,265,391** | **1,329,034** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHA 31/12/2022
(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| Mwaka Uliopita 31 Desemba 2021 | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | ziada ya kisheria | Upunguzaji wa jumla wa matengo | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2021** | **13,761,662** | **-** | **(11,636,136)** | **111,261** | **-** | **-** | **2,236,788** |
| Faida/(hasara) halisi baaada ya kodi ya mapato | | - | 293,551 | - | - | - | 293,551 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | 217,327 | - | - | - | - | - | 217,328 |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | 84,680 | (84,680) | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | | | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | | | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31.12.2020** | **13,978,989** | **-** | **(11,257,904)** | **26,581** | **-** | **-** | **2,747,668** |
| | | | | | | | |
| **Mwaka wa sasa 2022** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2022** | **13,978,989** | **-** | **(11,257,904)** | **26,581** | **-** | **-** | **2,747,668** |
| Faida/(hasara) halisi baaada ya kodi ya mapato | | - | 327,259 | - | - | - | 327,259 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | 1,326,163 | - | - | - | - | - | 1,326,163 |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | 92,038 | (92,038) | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | | | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | | | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31.12.2021** | **15,305,152** | **-** | **(10,838,607)** | **(65,457)** | **-** | **-** | **4,401,090** |

| *JINA NA CHEO* | SAINI | TAREHE |
|---|---|---|
| Godfrey J. Ng'urah **MENEJA MKUU** | | 4/14/23 |
| Kinyaki O. Kinyaki **MKUU WA FEDHA NA UTAWALA** | | 4/14/23 |
| Apolinary S. Kityamwi **MKUU WA UKAGUZI WA NDANI** | | 4/14/23 |

Ripoti ya mehesabu yaliyokaguliwa kwa mwaka ulioishia 31 Disemba, 2021 yameandaliwa kwa kutumia kanuni za mahesabu za kimataifa (IFRS). Ripoti hii ya mahesabu imekaguliwa na INNOVEX AUDITORS na kupatiwa hati safi. Taarifa za mahesabu zimeidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi tarehe 29 March, 2022 na kusaininwa kwa niaba na:-

| *JINA NA CHEO* | SAINI | TAREHE |
|---|---|---|
| 1. Dr GERVAS M. MACHIMU, MWENYEKITI WA BODI | | 4/14/23 |
| 2. CPA. MWAMINI J. MUSSA, MKURUGENZI | | 4/14/23 |

HABARI KIMATAIFA

# Rais mteule Nigeria kuapishwa Mei

**ABUJA,** Nigeria

WAZIRI wa Habari wa Nigeria Lai Mohammed amesema Rais mteule Bola Tinubu ataapishwa Mei 29, mwaka huu licha ya kesi inayoendelea mahakamani kupinga ushindi wake.

**Uchaguzi wa urais uliofanyika Februari 25, mwaka huu.**

Inaelezwa kuwa makundi ambayo hayajaridhishwa na matokeo ya uchaguzi wa urais uliofanyika Februari 25, mwaka huu nchini Nigeria yanaitisha serikali ya mpito huku Rais anayemaliza muda wake Muhammadu Buhari akiondoka madarakani rasmi mwezi Mei.

Waziri Mohammed alisema hakuna msingi wa katiba ya serikali ya mpito, akieleza kuwa vyama vya siasa vya upinzani vina haki ya kupinga uchaguzi wa urais mahakamani.

Awali wagombea wanne walioshiriki katika kinyang'anyiro cha kugombea urais nchini humo waliwasilisha mapingamizi ya kisheria Machi 21 mwaka huu, dhidi ya ushindi wa Rais mteule Tinubu, kwa madai kuwa kulikuwa na wizi wa kura na udanganyifu.

Aidha, inaelezwa kuwa inachukua takriban miezi minane kwa mahakama kuamua ombi la uchaguzi wa urais, na kwamba ombi hilo lazima lisikilizwe ndani ya siku 180 tangu siku lilipowasilishwa.

Hata hivyo, inaelezwa kuwa mlalamishi anaweza kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa mahakama katika Mahakama ya Rufaa ndani ya siku 21 kutoka tarehe ya uamuzi.

Vile vile, imebainishwa kuwa iwapo walalamikaji hawajaridhika na uamuzi wa mahakama ya rufaa, unaotolewa ndani ya siku 60, wana siku 21 za kukata rufaa katika Mahakama ya Juu, ambayo uamuzi wake ni wa mwisho. **BBC**

## Jeshi laonya hali ya hatari Sudan

**KHARTOUM,** Sudan

JESHI la ulinzi nchini Sudan limehadharisha juu la hali ya usalama nchini humo, baada ya kubaini kwamba kikosi chenye nguvu kilichoundwa na wanamgambo wa zamani cha (RSF) kinachoongozwa na Jenerali Mohamed Dagalo kimetawanywa katika maeneo mbalimbali ikiwemo mji mkuu wa Khartoum.

RSF ni kundi la wanamgambo wa zamani lenye nguvu ambalo limekuwa katika shutuma ya ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu, hasa wakati wa mzozo katika jimbo la Darfur nchini Sudan.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na jeshi hilo, hali hiyo inazusha hofu ya kutokea makabiliano ndani ya jeshi la Sudan.

Taarifa ilisema kitendo cha kikosi hicho chenye kuhusika na uingiliaji wa matuko ya dharura kinaonesha wazi ukiukwaji wa sheria za nchi hiyo.

Msemaji wa jeshi la Sudan Ali Mohammed, kupitia televisheni ya umma alisema vikosi vya jeshi kikatiba na kisheria vina jukumu la kulinda na kudumisha ulinzi na usalama wa nchi kwa msaada wa vyombo mbalimbali vya dola.

"Nchi yetu inapita katika mazingira hatari ya kihistoria, hatari zake zinaongezeka kwa amri ya RSF, kuhamasisha matumizi ya nguvu na kutawanywa ndani ya mji mkuu na baadhi ya miji," alisema Mohammed.

Pia inaelezwa kuwa uhusiano kati ya jeshi na kundi hilo la RSF umezidi kuzorota katika siku za hivi karibuni na kusababisha kucheleweshwa kwa kusainiwa kwa makubaliano yanayoungwa mkono kimataifa ya kuanza kwa siasa wakati wa kipindi cha miaka miwili ya serikali ya mpito wa kiraia kuelekea uchaguzi.

Vyanzo viwili vinasema kiini cha kutoelewana kati ya uongozi wa kundi hilo na jeshi ni hali ya kusitasita kutokuwa wazi katika uwekaji wa muda wa mwisho wa kuwaunganisha wapiganaji wa RSF na jeshi.

Katika taarifa ya kikosi hicho ambacho kinahudumu kwa uratibu wa sheria maalumu na kina mfumo wake chenyewe wa uongozi, kinasema kupeleka askari katika maeneo tofauti ya nchi, ni sehemu ya majukumu yake ya kwaida. **DW**



Maji yakionekana kuenea katika makazi ya watu nchini Burundi baada ya mafuriko yaliyotokea wiki iliyopita na kuwaacha maelfu ya watu bila makazi. **PICHA: DW**

## Wakenya wapatao 32 watupwa jela nchini Uganda

**KAMPALA,** Uganda

RAIA 32 wa Kenya wamehukumiwa kifungo cha miaka 10 na mahakama ya kijeshi ya Uganda yenye makao yake katika wilaya ya Moroto kaskazini mwa nchi hiyo.

Hiyo ni kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Naibu Msemaji wa Jeshi la Uganda, Kanali Deo Akiiki, akibainisha kuwa walipatikana na hatia ya kumiliki bunduki na risasi kinyume cha sheria, ikiwa ni makosa yanayoshitakiwa katika Mahakama ya Kijeshi nchini Uganda.

Ilielezwa kuwa kila kosa linasababisha kifungo cha miaka 10 jela, na kwamba mahakama hiyo iliamuru Jumatano ya wiki iliyopita kuwa raia hao watatakiwa kutumikia kifungo kwa wakati mmoja.

Wakenya wote ni wakazi wa kaunti ndogo ya Orum iliyopo katika wilaya ya Lodwar, katika Kaunti ya Turkana na walipatikana na hatia baada ya kukiri wenyewe, ikibainishwa kuwa watatumikia kifungo hicho katika gereza la serikali la Moroto.

Taarifa ilieleza kuwa Wakenya hao walikuwa ni miongoni mwa washitakiwa zaidi ya 100 waliokamatwa Aprili 8, mwaka huu kutoka kwenye maficho yao katika kijiji cha Lokeriaut kilichopo kaunti ndogo ya Nanduget wilayani Moroto Uganda.

Aidha, ilibainishwa kuwa jeshi hilo lilipata bunduki haramu 31 na risasi takribani 751 wakati wa operesheni ambayo ni sehemu ya zoezi la msako wa kuwapokonya silaha watu wanaozimiliki kinyume cha sheria. **BBC**

## Uchunguzi waanzishwa mauaji Afrika Kusini

**CAPE TOWN,** Afrika Kusini

POLISI nchini Afrika Kusini imesema uchunguzi umefunguliwa baada ya watu sita kuuawa kwa kupigwa risasi katika kitongoji cha wafanyakazi kilichopo karibu na mji wa Cape Town, huku kukiwa na madai kwamba tukio hilo ni ulipizaji kisasi.

Watu hao waliuawa Jumatano ya wiki iliyopita, katika shambulio lililotekelezwa na watu wenye silaha Afrika Kusini.

Taarifa ya polisi iliyotolewa jana ilisema washambuliaji hao wenye silaha waliegesha gari lao mbele ya jengo moja katika mji wa Ocean View, kwenye rasi ya kitalii ya Cape Town, na baada ya muda waliwafyatulia watu risasi hali iliyosababisha wanaume sita kuuawa.

"Uchunguzi umefunguliwa kwa mauaji, polisi wakishuku ulipizaji kisasi, kutokana na ushahidi wa kwanza uliokusanywa papo hapo, kuhusiana na shughuli za magenge, hakuna mtu aliyekamatwa na polisi wamewataka mashahidi kujitokeza," ilisema.

Chombo cha habari cha Democratic Alliance (DA) kilisema uchunguzi katika eneo hilo lenye idadi ndogo ya maofisa wa polisi, una hatari ya kuwa mgumu zaidi kutokana na kwamba kamera za usalama (CCTV) zilizimwa wakati wa shambulio hilo. **RFI**

# JEMBE ULAYA AWATABIRIA MAKUBWA BALEKE, AZIZ KI

**Na Shufaa Lyimo**

NYOTA wa zamani wa Yanga, Bakari Malima 'Jembe Ulaya' amesema mechi ya watani wa jadi nchini, Simba na Yanga itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam itakuwa na 'mvuto mkubwa' kutokana na aina ya usajili uliofanywa na timu hizo.

Simba itakuwa mwenyeji wa mechi hiyo ya marudiano ya Ligi Kuu Tanzania Bara na mshindi atakuwa amejisafishia njia ya ubingwa wa msimu huu.

**Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Jembe Ulaya alisema anaamini mechi hiyo itakuwa na ushindani na si nyepesi kwa upande wowote.**

Jembe Ulaya alisema kila timu itatakuwa kuwa makini katika muda wote kwa sababu lolote linaweza kutokea ndani ya dakika hizo 90.

"Mchezo wa Simba na Yanga wa Jumapili unatarajiwa kuwa na mvuto wa aina yake kutokana na aina ya vikosi vilivyo sasa, timu zote zimeimarika kwa kiasi kikubwa tofauti na zilivyokuwa miaka ya nyuma, zimesajili wachezaji ambao wana viwango vya kimataifa na wanaocheza soka la ushindani," alisema Jembe Ulaya.

Nyota huyo ambaye kwa sasa anaifundisha timu ya vijana ya Yanga, alisema kwa upande wa Simba imeimarika zaidi baada ya kuwasajili wachezaji wa kimataifa, Saidi Ntibazonkiza na Jean Baleke, ambao wameongeza nguvu kwenye safu ya ushambuliaji.

"Sina mashaka na kikosi cha Yanga baada ya kumwona, Stephano Aziz Ki amerudi kwenye kiwango chake cha kawaida, tunaomba mashabiki wajitokeze kwa wingi uwanjani kuangalia burudani itakayotolewa na wachezaji wetu siku hiyo," mkongwe huyo alisema.

Timu hizo zinakutana zote zikiwa zimetinga hatua ya robo fainali ya mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).




Mashabiki wa Yanga wakionyesha ishara ya tano baada ya timu yao kupata ushindi wa mabao 5-0 katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Kagera Sugar iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: MTANDAO**

# *Jamhuri Kihwelo 'Julio' mrithi wa Hitimana KMC*

**Na Saada Akida**

MABOSI wa KMC FC wamemtangaza, Jamhuri Kihwelo 'Julio' kuwa kocha mpya wa timu hiyo akichukua nafasi ya Thierry Hitimana, imeelezwa.

Uongozi wa timu hiyo umefikia uamuzi huo kutokana na mwenendo mbaya wa KMC katika msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambao unaelekea ukingoni.

Akizungumza na gazeti hili jana, Hitimana alisema ni kweli alipokea barua kutoka kwa viongozi wa klabu hiyo ya kusitisha mkataba wake.

Hitimana, kocha wa zamani wa Simba, Mtibwa Sugar na Namungo, alisema amekubaliana na uamuzi wa viongozi wa klabu hiyo na kuwataka wamlipe stahiki zake.

"Ni kweli wamenipa barua inayonitaka nisiwepo katika benchi la ufundi ndani ya siku saba kuanzia jana (juzi), nami nimewataka tumalizane kwa kusitisha mkataba, sasa nasubiri kupewa haki zangu na kuangalia changamoto nyingine," alisema kocha huyo ambaye aliwahi kufanya kazi Namungo, Mtibwa Sugar na Simba.



## Bunge laipongeza Fountain Gate

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetakiwa 'kuzitazama vizuri sana' timu za soka za wanawake katika ngazi zote kutokana na kufanya vizuri katika mashindano mbalimbali wanayoshiriki, imeelezwa.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson wakati akiipongeza timu ya wasichana ya Shule ya Sekondani ya Fountain Gate Dodoma iliyotwaa ubingwa wa Afrika katika mashindano yaliyofanyika Durban, Afrika Kusini hivi karibuni.

Akitambulisha timu hiyo bungeni jana, iliyoambatana na viongozi wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Tulia alisema timu hiyo imefanya vizuri na wameliheshimisha taifa.

"Sasa hivi sawa tunajua Simba na Yanga wanafanya vizuri kimataifa lakini tunawatakia kila la heri walete mambo mazuri kama haya, timu hizi mzitazame vizuri sana, wameonyesha mfano mzuri na huko mbeleni tunakwenda kuwa na kikosi kizuri cha timu ya wanawake," Tulia alisema.

Fountain Gate ambao pia ni mabingwa wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), imetwaa ubingwa wa kwanza wa mashindano hayo yaliyoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF) na kutwaa kitita cha Dola za Marekani 300,000.

## Alliance Girls FC roho ya Mwanza

**Na Jofrey Kobeto,** SAUT

WAKATI mashabiki wa soka wa Mwanza wakitamba tegemeo pekee kwao kwa sasa ni Alliance Girls inayoshiriki Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, viongozi wa timu hiyo wamesema wanaendelea kujipanga kuhakikisha wanalipa heshima jiji hilo.

Kauli hiyo imetolea siku chake baada ya Alliance Girls kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Yanga Princess kutoka Dar es Salaam.

"Hivi karibuni tumeona wakiwashushia Yanga kichapo cha bao 1-0, katika msimamo wako kwenye nafasi ya tano baada ya kufikisha pointi 20, matokeo yao yanaturidhisha sisi mashabiki," alisema Hamis Hussein, mdau wa soka wa timu hiyo.

Naye Ofisa Habari wa Alliance Girls, Asia Jumanne, alisema timu yao inaendelea kujiimarisha kuhakikisha wanaonyesha ushindani katika kila mechi ya ligi wanayocheza.

"Licha ya changamoto tunazopitia lakini tumejipanga ipasavyo kuhakikisha timu inakuwa kubwa na tishio, vijana wetu wengi ni watoto tuliowalea sisi na wana vipaji vikubwa, tunajitahidi kuwasimamia si kwa ajili ya Alliance tu bali ni kwa hazina ya taifa kwa ujumla," alisema Asia.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### CITY KUMNASA BELLINGHAM

KLABU ya Manchester City inaongoza dhidi ya Real Madrid katika kinyang'anyiro cha kumnunua mchezaji wa Borussia Dortmund, Jude Bellingham, baada ya Liverpool kujiondoa kumsajili kiungo huyo wa kati wa England mwenye umri wa miaka 19. ***(ESPN)***

### LIVERPOOL YASAKA KIUNGO

NYOTA wa West Ham na England, Declan Rice, 24, mchezaji wa kimataifa wa Ecuador, Moises Caicedo (21), nyota wa Inter Milan na Italia, Nicolo Barella (26) na mchezaji wa Wolves na Ureno, Matheus Nunes (24), wamebakia kwenye orodha ya Liverpool inayomsaka kiungo mpya. ***(Florian Plettenberg)***

### GUNDOGAN ANUKIA BARCA

BARCELONA itazidisha nia ya kumnunua, Ilkay Gundogan, 32, baada ya kufurahishwa na mchezo wa kiungo huyo wa kati Mjerumani akiwa na Manchester City dhidi ya Bayern Munich kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Sport)***

### GRAVENBERCH AGOMBEWA

KLABU ya Arsenal, Liverpool na Manchester United zinamfuatilia kiungo wa kati wa Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Ryan Gravenberch, 20. ***(Footmercato)***

### SLOT AGEUKA LULU

KLABU za Tottenham, West Ham na Crystal Palace zote zinamtaka Kocha Mholanzi Arne Slot, ambaye ameigeuza Feyenoord kuwa viongozi wa Ligi Kuu ya Uholanzi maarufu Eredivisie. ***(Times)***

### VILLA, PALACE VITANI

FULHAM, Aston Villa na Crystal Palace zinavutiwa na kiungo wa kati wa Besiktas na Timu ya Taifa ya Ureno, Gedson Fernandes, 24. ***(Calciomercato)***

### PALHINHA KUTUA LIVERPOOL

LIVERPOOL imetuma maskauti kumwangalia kiungo wa kati wa Fulham, Joao Palhinha, mara kadhaa wakifikiria kumnunua mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno mwenye umri wa miaka 27 ifikapo msimu wa joto. ***(Football Insider)***

### HEGERBERG KUTUA BARCA

TIMU ya soka ya wanawake ya Barcelona itajaribu tena kumsajili mshambuliaji wa Lyon na Norway, Ada Hegerberg, 27, huku klabu hiyo ya Hispania ikiwa tayari kutoa ada ya kuvunja rekodi ya dunia ya pauni 420,000 kwa mchezaji huyo. ***(90min)***

### SMALLING MAMBO SAFI

MLINZI wa zamani wa England, Chris Smalling, 33, anatarajia kutiasaini mkataba mpya wa miaka miwili katika klabu ya AS Roma wiki hii licha ya nia ya kutakiwa na Inter Milan, Juventus na klabu kadhaa za Ligi Kuu England. ***(Sport)***

### ARSENAL KUMUUZA BALOGUN

ARSENAL itadai pauni milioni 35 kwa mshambuliaji wa England, Folarin Balogun, 21, ambaye kwa sasa yupo kwa mkopo kule Reims na analengwa na RB Leipzig. ***(Florian Plettenberg)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# VINICIUS: REAL MADRID TUMEONYESHA UBORA

**MADRID,** Hispania

### ●●● Yajipanga kukabiliana na ushindani ikiifuata Chelsea katika mechi...

VINICIUS Junior amesifu kiwango cha Real Madrid dhidi ya Chelsea kama moja ya ubora wao msimu huu, huku mabingwa hao watetezi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya wakiibuka na ushindi wa mabao 2-0 katika mchezo wa kwanza wa hatua ya robo fainali uliochezwa juzi usiku.

**Madrid waliiondoa Chelsea katika hatua hii mwaka uliopita, ingawa kwa tofauti nzuri tu.**

Lakini wakati huu walikuwa wakipewa nafasi kubwa dhidi ya timu inayong'ang'ania nusu ya mwisho ya msimamo wa Ligi Kuu England na tofauti kati ya pande hizo mbili ilioneshwa uwanjani.

Chelsea walipata nafasi zao, huku golikipa Thibaut Courtois akiokoa hatari mara tatu, lakini Kipa Arrizabalaga alijikuta akitoa mpira ndani ya nyavu zake mara mbili.

Karim Benzema alifunga bao la kwanza kabla ya kumtengenezea tena pande Marco Asensio aliyefunga bao la pili dakika ya 74.

"Tulicheza vizuri sana, tukijitahidi kila wakati kama tulivyofanya katika hatua hii msimu uliopita," alisema Vinicius akinukuliwa na UEFA.com.

"Hii ilikuwa moja ya kiwango chetu bora msimu huu.

"Lakini hii ni muda wa mapumziko tu. Kuna mengi yamesalia katika sare hii. Tunahitaji tu kuweka vichwa vya watu watulivu."

Madrid walicheza zaidi ya nusu saa dhidi ya wachezaji 10 baada ya Ben Chilwell kutolewa nje kwa kadi nyekundu.

"Kulikuwa na nafasi nyingi kwa sisi kusukuma ndani, na ni wazi Real Madrid tunataka kufunga mabao zaidi kila wakati," aliongeza Vinicius.

"Tunajua kwamba mechi ya ugenini dhidi ya Chelsea inaweza kuwa ngumu. Sasa tunapumzika kidogo na kuweka kichwa sawa."

Madrid ilikaa kwa miaka mitatu bila ushindi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya Vinicius kusajiliwa, lakini sasa anatazamia kutwaa taji la pili mfululizo kama klabu yenye mafanikio zaidi kwenye michuano hiyo ikilenga kutwaa taji la 15.

"Mchezaji yeyote anayevaa jezi hii kwa Madrid anajua jinsi Ligi ya Mabingwa Ulaya ilivyo maalum," alisema.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,102,0

MECHI KALI

SPEZIA
VERSUS
LAZIO

1 | 4.61
X | 3.50
2 | 1.70

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom | m-pesa
halopesa
airtel money

SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# CHELSEA WANA NAFASI NUSU FAINALI - LAMPARD



**MADRID,** Hispania

FRANK Lampard alisisitiza "mlango uko wazi" kwa Chelsea kufika hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini akaongeza watahitaji "usiku maalum" kule Stamford Bridge kutafuta njia ya kuwaondoa Real Madrid.

Madrid walichukua udhibiti wa mchezo wao wa kwanza wa robo fainali Jumatano huku mabao ya Karim Benzema na Marco Asensio yakiipa timu hiyo ya Carlo Ancelotti ushindi wa magoli 2-0 dhidi ya The Blues hao, ambao walicheza nusu saa ya mwisho wakiwa na wachezaji 10 kufuatia kadi nyekundu ya Ben Chilwell kwa kumwangusha Rodrygo.

Chelsea hawakuwa na bahati ya kushindwa na Lampard anaamini nafasi bado ipo ya kutinga hatua ya nne bora katika mechi ya mkondo wa pili itakayochezwa Jumanne ijayo.

"Nadhani ni changamoto kubwa, bila shaka, dhidi ya timu yenye ubora kama Real Madrid," alisema Lampard.

"Lakini mlango uko wazi na ni juu yetu ikiwa tunataka kuufungua zaidi wiki ijayo au la.

"Matokeo ndio ukweli. Nimewaambia wachezaji 'mambo maalum yanaweza kutokea Stamford Bridge.' Ni timu nzuri sana lakini tunapaswa kuamini."



## Bellingham sasa akaribia City

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester City inaongoza katika kinyang'anyiro cha kumnunua Jude Bellingham baada ya Liverpool kujitoa kumwania kiungo huyo wa kati wa England, vyanzo vimeambia ESPN.

Real Madrid bado wanavutiwa na Bellingham, lakini City wanazidi kujiamini wanaweza kumpata kinda huyo mwenye umri wa miaka 19 kutoka Borussia Dortmund.

City wanasaka sana kusajili angalau kiungo mmoja katika dirisha la majira ya joto kwa sababu ya mashaka juu ya mustakabali wa muda mrefu wa Ilkay Gundogan, ambaye mkataba wake unatarajiwa kumalizika ifikapo Juni na Bernardo Silva.

Uhamisho wa Bellingham huenda ukagharimu zaidi ya pauni milioni 130, ingawa Dortmund haijakata tamaa ya kumbakiza kinda huyo kwa msimu mmoja zaidi.

Bellingham hivi majuzi alishika nafasi ya kwanza kwa wachezaji 39 bora wa kiume wa ESPN wenye umri wa miaka 21, baada ya kuichezea Dortmund tangu ajiunge na klabu hiyo mwaka wa 2020.

Aliongeza kiwango chake zaidi kwa mfululizo wa maonyesho ya kuvutia kwa England walipotinga robo fainali ya Kombe la Dunia 2022.

82,037/-

# JOTO LAPANDA KUELEKEA MECHI YA SIMBA, YANGA

**Na Adam Fungamwango**

JOTO linazidi kupanda kuelekea mechi ya watani wa jadi nchini, Simba na Yanga itakayochezwa Jumapili baada ya kila upande kutamba wameimarika na wako tayari kwa mtanange huo utakaopigwa kuanzia saa 11:00 jioni kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Timu hizo zitakutana zikiwa na kumbukumbu ya sare ya bao 1-1 waliyopata katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, mzunguko wa kwanza iliyochezwa Oktoba 23, mwaka jana.**

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, ametamba kwa ubora wa kikosi walichonacho wataendeleza umwamba wao wa mara kwa mara dhidi ya Simba.

"Sisi Yanga hatumung'unyi maneno, tunautaka ubingwa wa Tanzania Bara, lakini hautonoga kama hatujamkanda mnyama siku ya Jumapili, maandalizi yameshaanza na kambi tumeianza. Cha kufurahisha ni wenyewe wameanza kuwa na wasiwasi.

Wanaanza kuwahimiza wachezaji wao waende kucheza mechi ya kufa, mechi ya jasho na damu waingie kwenye vitabu vya historia ya kuifunga Yanga, hapo unaweza kuona utofauti kati yao na yetu, sisi malengo yetu msimu huu ni kuchukua ubingwa, lakini wao ni kuifunga Yanga, tunawaambia hivi, hakuna timu ya kutufunga Jumapili," alisema Kamwe.

Naye Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, amewataka wachezaji wa Simba kuwaondolea unyonge wanachama na mashabiki wao.

"Mchezo huu sisi ni wa thamani na maana kubwa, ukubwa wake haujawahi kumithilika, kwa sababu kwanza ni 'dabi' na heshima ya klabu yoyote ni kushinda 'dabi.' Simba kwa muda mrefu hatujaifunga Yanga kwenye mechi ya watani wa jadi, mara ya mwisho kumbukumbu zinaeleza kuwa tulipata ushindi wa bao 1-0 mwaka 2019 kwa sasa ni miaka mitatu imepita, ili upate heshima ya kutosha kwa mchezaji na kocha ni lazima upate ushindi kwenye mechi kama hizi," Ahmed alisema.



Ali Kamwe



Ahmed Ally

## Nabi amkabidhi majukumu

INATOKA UK. 24

huyo.

Aliongeza safu ya ulinzi ya timu hiyo itakuwa na mabadiliko kidogo kutokana na ubora wa wapinzani wao na umuhimu wa mechi hiyo.

"Unaona sasa tuna wigo mpana wa kuchagua nani wa kuanza katika upande wa mabeki wa kati, lakini kwangu Bacca amekuja vizuri, ameonyesha uwajibikaji mkubwa. Kazi kubwa ni kutumia hizi siku kufanya maandalizi mazuri na kulingana na ubora wa wapinzani wetu, kuhusu safu ya ulinzi kumekuwa na ushindani mkubwa hasa kuonyesha kiwango kuzuri kwa Ibrahim Abdallah (Bacca)," alisema.

Kocha huyo alisema wala hawana presha yoyote sasa watakuwa na wigo mpana wa kuchagua nani yuko sawa kulingana na mpinzani wanayekwenda kukutana naye.

Aliongeza Bacca ameonyesha uimara mkubwa tangu aanze kupewa nafasi amemtaka sasa kubaki katika muendelezo wa kiwango chake huku akiwataka wenzake nao kuendelea kujipanga sawasawa.

"Sidhani kama kuna changamoto, kazi yetu kama makocha ni kuchagua nani anafaa kuanza katika kikosi cha kwanza," alisema kocha huyo.

## *Kibadeni awafunda*

INATOKA UKURASA 24

kea mchezo wetu dhidi ya Yanga, safari hii hatutakubali kupoteza mchezo huu, ninaimani wachezaji wakijituma na kupambana, Yanga hata tucheze nao siku mbili hawatufungi," alisema Ahmed.

Alisema pia Mwekezaji wa klabu hiyo, Mohammed Dewji 'Mo' amemteua, Hussein Kitta, kuwa mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, ambapo awali alikuwa mjumbe kupitia upande wa wanachama.

Kitta anaungana na Dk. Raphael Chegeni, Hamza Johari, Zulfikar Chandoo na Rashid Shangazi huku wajumbe waliochaguliwa ni Asha Baraka, Suleiman Haroub, Dk. Seif Muba na Rodney Chiduo.



## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 15/04/23 | 17:00 | Wolverhampton Wanderers vs Brentford FC | 2.33 | 3.10 | 2.95 |
| 02. 15/04/23 | 17:00 | Chelsea FC vs Brighton & Hove Albion | 2.41 | 3.25 | 2.75 |
| 03. 15/04/23 | 17:00 | Southampton FC vs Crystal Palace | 2.60 | 3.10 | 2.60 |
| 04. 15/04/23 | 17:00 | Blackpool vs Wigan Athletic | 2.35 | 3.05 | 3.00 |
| 05. 15/04/23 | 17:00 | Queens Park Rangers vs Coventry City | 2.90 | 3.00 | 2.41 |
| 06. 15/04/23 | 17:00 | Stoke City vs West Bromwich Albion | 2.55 | 3.10 | 2.65 |
| 07. 15/04/23 | 17:00 | KAS Eupen vs SV Zulte Waregem | 2.33 | 3.40 | 2.75 |
| 08. 15/04/23 | 17:30 | Estoril Praia vs Portimonense SC | 2.38 | 3.00 | 3.00 |
| 09. 15/04/23 | 18:00 | Stade Rennes vs Stade Reims | 2.22 | 3.30 | 2.95 |
| 10. 15/04/23 | 19:15 | KV Oostende vs Oud-Heverlee Leuven | 2.48 | 3.45 | 2.50 |
| 11. 15/04/23 | 22:00 | Sparta Rotterdam vs SC Heerenveen | 2.23 | 3.30 | 2.95 |
| 12. 15/04/23 | 22:00 | America FC MG vs Fluminense FC RJ | 2.70 | 3.10 | 2.55 |
| 13. 16/04/23 | 00:30 | Botafogo FR RJ vs Sao Paulo FC SP | 2.49 | 3.05 | 2.80 |
| 14. 16/04/23 | 03:30 | Gimnasia Y Esgrima La Plata vs CA Belgrano | 2.30 | 2.75 | 2.90 |
| 15. 16/04/23 | 19:30 | Malaga CF vs FC Cartagena | 2.31 | 2.90 | 3.20 |
| 16. 16/04/23 | 20:00 | Union de Santa Fe vs CA Tigre | 2.60 | 2.85 | 2.47 |
| 17. 16/04/23 | 20:30 | VfL Wolfsburg vs Bayer Leverkusen | 2.75 | 3.35 | 2.32 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### IJUMAA - 14/04/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 3469 | Rukh Vinnyky vs Dynamo Kiev | 6.16 | 4.31 | 1.40 |
| 15:00 | 4785 | Dire Dawa Kenema FC vs Bahir Dar Kenema FC | 4.55 | 3.62 | 1.66 |
| 16:00 | 1327 | Hapoel Petah Tikva vs Hapoel Acre | 1.62 | 3.85 | 4.96 |
| 16:00 | 2442 | Ironi Tiberias vs Maccabi Petach Tikva | 2.21 | 3.10 | 2.75 |
| 16:30 | 1423 | Kustosija vs Rudes Zagreb | 4.32 | 3.24 | 1.76 |
| 16:30 | 2391 | Barito Putera vs Persita Tangerang | 1.81 | 3.58 | 3.58 |
| 16:30 | 3595 | Arema vs Bhayangkara Surabaya Utd | 1.92 | 3.40 | 3.40 |
| 18:00 | 1442 | Viktoria Otrokovice vs Znojmo | 2.22 | 3.84 | 2.57 |
| 19:00 | 2523 | HNK Sibenik vs HNK Gorica | 2.47 | 3.09 | 2.62 |
| 19:30 | 1516 | Cremonese vs Empoli | 2.45 | 3.15 | 2.75 |
| 19:30 | 5022 | Hannover vs Heidenheim | 3.12 | 3.38 | 2.16 |
| 19:30 | 5714 | Greuther Furth vs Jahn Regensburg | 1.77 | 3.64 | 4.15 |
| 20:00 | 1289 | Midtjylland vs Aalborg | 1.71 | 3.76 | 4.47 |
| 20:00 | 2752 | Saarbrucken vs Dynamo Dresden | 2.41 | 3.49 | 2.64 |
| 20:00 | 5341 | Oliveirense vs Sporting Farense | 2.97 | 3.23 | 2.23 |
| 20:00 | 5363 | Sonderjyske vs Vendsyssel FF | 1.77 | 3.59 | 3.74 |
| 20:30 | 1975 | Bastia Borgo vs Sedan | 3.21 | 3.21 | 2.17 |
| 20:30 | 2351 | Antalyaspor vs Alanyaspor | 1.95 | 3.53 | 3.47 |
| 20:30 | 3531 | Galatasaray vs Kayserispor | 1.28 | 5.43 | 8.15 |
| 20:30 | 3579 | Dunkerque vs Avranches | 1.94 | 3.37 | 3.68 |
| 20:30 | 4493 | Le Mans vs Chateauroux | 2.26 | 3.14 | 3.09 |
| 20:30 | 4495 | FC Schaffhausen vs Yverdon-Sport FC | 2.62 | 3.24 | 2.38 |
| 20:30 | 4809 | Bourg Peronnas vs Le Puy | 2.07 | 3.26 | 3.37 |
| 21:00 | 1385 | VVV Venlo vs FC Eindhoven | 2.16 | 3.33 | 3.01 |
| 21:00 | 2667 | SBV Excelsior vs GO Ahead Eagles | 3.06 | 3.36 | 2.15 |
| 21:00 | 2900 | UTA Arad vs Botosani | 2.05 | 3.14 | 3.51 |
| 21:00 | 5671 | PEC Zwolle vs Telstar | 1.25 | 5.61 | 8.73 |
| 21:15 | 5669 | FC Thun vs FC Aarau | 1.76 | 3.79 | 3.59 |
| 21:15 | 5915 | Luka Koper vs ND Gorica | 1.85 | 3.39 | 3.65 |
| 21:30 | 1791 | Schalke 04 vs Hertha BSC | 2.28 | 3.25 | 2.90 |
| 21:30 | 3587 | Modena vs Parma | 2.82 | 3.09 | 2.43 |
| 21:45 | 1315 | Athlone Town vs Cobh Ramblers | 2.28 | 3.29 | 2.72 |
| 21:45 | 1894 | Bala Town vs The New Saints | 7.26 | 4.77 | 1.33 |
| 21:45 | 2368 | Bohemians FC vs St Patricks | 2.19 | 3.14 | 2.99 |
| 21:45 | 2959 | UCD Dublin vs Cork City | 3.96 | 3.39 | 1.78 |
| 21:45 | 3246 | Galway United vs Bray Wanderers | 1.39 | 4.19 | 6.55 |
| 21:45 | 4405 | Ross County vs Aberdeen | 3.12 | 3.32 | 2.16 |
| 21:45 | 4594 | Queens Park vs Hamilton | 1.54 | 4.12 | 4.90 |
| 21:45 | 4901 | Al-Sailiya SC vs Al Rayyan SC | 3.80 | 3.60 | 1.76 |
| 21:45 | 4924 | Shamrock Rovers vs Shelbourne | 1.53 | 3.60 | 5.56 |
| 21:45 | 5051 | Standard Liege vs Charleroi | 1.97 | 3.47 | 3.47 |
| 21:45 | 5760 | Spezia vs Lazio | 4.61 | 3.50 | 1.70 |
| 22:00 | 1609 | Middlesbrough vs Norwich City | 1.90 | 3.55 | 3.55 |
| 22:00 | 2811 | Albacete Balompie vs Eibar | 2.66 | 2.91 | 2.71 |
| 22:00 | 3564 | Toulouse vs Lyon | 2.70 | 3.60 | 2.27 |
| 22:00 | 3833 | Rayo Vallecano vs Osasuna | 2.08 | 3.10 | 3.50 |
| 22:15 | 1399 | Aswan vs Pyramids | 5.83 | 3.52 | 1.59 |
| 22:15 | 2321 | El Ittihad Alexandria vs Smouha Club | 2.23 | 3.02 | 3.27 |
| 22:15 | 4054 | Al Ahly Cairo vs Farco FC | 1.32 | 4.42 | 9.64 |
| 22:15 | 5612 | Famalicao vs Vitoria Guimaraes | 2.16 | 3.07 | 3.37 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Ijumaa Aprili 14, 2023

Nipashe




‘Madrid tumeonyesha ubora’ UKURASA 21



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (mwenye suti ya bluu), akipokea kikombe cha ubingwa wa mashindano ya Wasichana ya Shule za Sekondari Afrika kutoka kwa nahodha wa Fountain Gate baada ya kualikwa bungeni Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kibadeni awafunda Simba

## Awataka wasikubali kuwa ‘ngazi’ Jumapili, atamani kuzikwa na rekodi ya...

**Hadija Mngwai na Saada Akida**

KOCHA na mshambuliaji wa zamani wa Wekundu wa Msimbazi, Abdallah Kibadeni ‘King’ ameitaka timu hiyo kuhakikisha inapata ushindi katika mechi dhidi ya watani zao, Yanga na kuchelewesha sherehe zao za kutangaza ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

**Simba inatarajia kuikaribisha Yanga katika mechi ya marudiano ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Jumapili kuanzia saa 11:00 jioni kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.**

Yanga yenye pointi 68 inaongoza katika msimamo wa ligi hiyo yenye timu 16 ikifuatiwa na Simba yenye pointi 60 wakati Polisi Tanzania wanaburuza mkia na pointi zao 19.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Kibadeni alisema anaamini bado mbio za kuwania ubingwa ziko wazi na mechi hiyo inaweza kutoa picha tofauti na matarajio yaliyoko sasa.

Kibadeni alisema Simba inatakiwa kupambana kupata matokeo mazuri na kurejesha matumaini ya kushinda taji hilo kwa sababu wapinzani wao hawana uhakika wa kushinda mechi zote zilizosalia za ligi hiyo.

Kocha huyo amewataka wachezaji wa Simba kuonyesha upinzani na kurekebisha makosa waliyokuwa nayo ili wapate ushindi na kuwapunguza kasi mabingwa hao watetezi.

“Mechi ya Simba na Yanga ni mechi kubwa na itakuwa na upinzani mkubwa sana, hivyo ni suala la kujipanga hasa kwa upande wa Simba wahakikishe wanafuta yale makosa yaliyojitokeza katika mechi zilizopita walizocheza na timu nyingine. Wakifanya tena makosa kwa Yanga wajue watapoteza, wahakikishe wanafunga kwa sababu Yanga wakiwafunga watachukua ubingwa huo mapema, angalau wawacheleweshe,” Kibadeni alisema.

Aliongeza endapo Yanga itapoteza mechi huko mbele lolote linaweza kutokea lakini pia akiwataka nyota wa klabu hizo kongwe kuonyesha soka zuri ili timu nyingine zijifunze kupitia wao.

Kuhusu hat-trick aliyofunga mwaka 1977 dhidi ya Yanga katika ushindi wa mabao 6-0, alisema anaendelea kujisikia fahari kwa rekodi hiyo kutovunjwa hadi sasa.

“Ningeshukuru sana kuona Simba wangenipongeza kufuatia rekodi yangu ya kufunga hat-trick katika mechi dhidi ya Yanga kutovunjwa hadi sasa, ilikuwa mechi ngumu kweli kweli, kufunga mabao yote hayo halikuwa jambo dogo. Kwa kipindi hiki ni ngumu kidogo kwa mtu mmoja kufunga goli tatu peke yake hasa ukizingatia wanacheza wachezaji tofauti tofauti, ila naomba Mungu asitokee mtu yoyote wa kufunga hat-trick, naomba nife nayo ili rekodi yangu iweze kuendelea,” alimaliza nyota huyo.

Katika mechi hiyo Kibadeni alifunga bao la kwanza, la pili na la sita.

Naye Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, msimu huu wamedhamiria kuweka heshima na kuwapa furaha wanachama na mashabiki wa klabu hiyo kwa kupata ushindi hapo Jumapili.

“Bodi ilikutana na kujadili masuala mbalimbali ya

INAENDELEA UKURASA 23

# Nabi amkabidhi majukumu Bacca Jumapili

**Na Saada Akida**

KUTOKANA na kuimarika kwa safu ya ushambuliaji ya Simba, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amelazimika kuongeza dozi ya mazoezi katika safu yake ya ulinzi ili kuhakikisha wanakuwa salama kwenye mechi ya watani wa jadi itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Mbali na kuimarisha safu ya ulinzi, Yanga pia inajiweka sawa kwa kufanya mazoezi ya viungo gym kwa lengo la kuwa imara kuhakikisha wanafanya vizuri katika mechi hiyo.

Nabi aliliambia gazeti hili kazi nyingine anayoifanya ni kuzungumza na wachezaji wake na kuwaandaa kisaikolojia namna ya kuwadhibiti Simba huku akiwaeleza ubora na madhaifu ya wapinzani wao.

Kocha huyo alisema pia anawapa maelekezo washambuliaji wake namna maalum ya kufunga mabao ya mapema ili kuwaondoa Simba mchezoni.

“Kazi kubwa ni kutumia hizi siku zilizobaki kufanya maandalizi mazuri na kulingana na ubora wa wapinzani wetu, kuhusu safu ya ulinzi kumekuwa na ushindini mkubwa hasa kutokana na kiwango kizuri kilichoonyeshwa na Bacca (Ibrahim Abdallah),” alisema kocha huyo.

Aliongeza kikosi chake kitashuka dimbani bila presha yoyote na watakuwa na wigo mpana wa kuchagua kikosi cha kuanza katika mechi hiyo kulingana na mpinzani wanayekutana naye.

“Bacca ameonyesha uimara mkubwa tangu aanze kupewa nafasi, nataka kumwona anabakia katika mwendelezo wa kiwango chake, pia nawataka wachezaji wote kuendelea kujipanga sawasawa. Sidhani kama kuna changamoto, kazi yetu kama makocha ni kuchagua nani anafaa kuanza, tukijiridhisha juu ya uimara wa mchezaji kulingana na mpinzani tunayekwenda kukutana

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >